JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

---

# SHERIA YA MTOTO
[SURA YA 13]

# TAFSIRI YA KANUNI ZA USALAMA WA MTOTO ZA MWAKA 2014

Toleo hili la Kanuni za Malezi ya Kambo za mwaka 2012, Tangazo la Serikali Na. 11 la tarehe 4 Mei, Mwaka 2012, ni Tafsiri rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Mbalimbali, Sura ya 1.

Dar es Salaam
28 April, 2016

GEORGE M. MASAJU,
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 169 la tarehe 13/05/2016

# KANUNI ZA USALAMA WA WATOTO ZA MWAKA 2014

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MISINGI YA JUMLA NA VIWANGO

3. Misingi ya jumla na viwango.
4. Mtoto anayehitaji ulinzi.
5. Vigezo vya ulinzi wa mtoto.

SEHEMU YA TATU
MAJUKUMU YA JUMLA YA IDARA YA USTAWI WA JAMII

6. Kuanzishwa kwa idara ya ustawi wa jamii.
7. Majukumu ya idara ya ustawi wa jamii.
8. Kukuza uelewa wa jamii.
9. Melezo kwa wanataaluma.

SEHEMU YA NNE
RUFAA KUHUSU USALAMA WA MTOTO

10. Afisa mapokezi wa ustawi wa jamii.
11. Rufaa ya mtotot aliyeletwa na mwanajamii.
12. Rufaa ya motto kutoka kwa mtaalam.
13. Utaratibu baada ya kupokelewa kwa rufaa za usalama wa mtoto.

SEHEMUYA TANO
UCHUNGUZI WA AWALI

14. Kufanya uchunguzi wa awali.
15. Uchunguzi wa awali unaofanywa kwa pamoja na Polisi.

16. Kumhoji mtoto wakati wakati wa uchunguzi.
17. Kukubalika kwa ushahidi wa kusikia na kuona.
18. Kushindwa kufanya motto apatikane wakati wa uchunguzi.
19. Amri ya kutafuta na kuonyesha.
20. Mzazi kutoridhia uchunguzi wa kitabibu.
21. Mtoto kuridhia uchunguzi wa kitabibu.

SEHEMU YA SITA
HUKUMU

22. Kumwekea motto mahali salama.
23. Kuongeza muda wa kukaa kwenye sehemu ya usalama.

SEHEMU YA SABA
HATUA KUFUATIA UCHUNGUZI

24. Hatua kufuatia uchunguzi.
25. Kumtaarifu mrufaniwa kuhusu hatua zitakzochukuliwa.
26. Utaratibu iwapo kuna sababu ya kutiliwa shaka baada ya uchunguzi.

SEHEMU YA NANE
MKUTANO KUHUSU USALAMA WA MTOTO

27. Mkutano wa usalama wa mtoto.
28. Ushiriki wa motto na ndugu katika mkutano wa usalama wa mtoto.
29. Taarifa kwenye mkutano wa usalama wa mtoto.
30. Mwenyekiti wa mkutano wa usalama wa mtoto.
31. Wajibu wa mwenyekiti. Wa mkutano wa usalama wa mtoto.
32. Majadiliano ya kitaalam kwenye mkutano wa usalama wa mtoto.
33. Mukhtasari kwenye mkutano wa usalama wa mtoto.
34. Nyaraka kwenye mwenendo wa mkutano wa usalama wa mtoto.
35. Maamuzi ya mkutano wa usalama wa mtoto.
36. Mpango wa usalama wa mtoto.
37. Mapitio ya mpango wa usalama wa mtoto.

SEHEMU YA TISA
WATOTO WANAOHITAJI MSAADA NA MALAZI

38. Wajibu kwa watoto waliopotea, waliotekelezwa, wanaohitaji hifadhi au wasio na uangalizi wa wazazi.
39. Rufaa ya mtoto anayevunja sheria.

40. Uangalizi wa motto anayevunja sheria.
41. Wajibu kwa motto aliyehamishwa.
42. Kuwekwa chini ya uangalizi wakujitolea.
43. Kusitishwa kwa huduma ya uangalizi wa hiari.

SEHEMU YA KUMI
MAOMBI YA AMRI YA UANGALIZI AU USIMAMIZI

44. Maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi.

45. Mamlaka ya kuomba ya amri ya uangalizi au usimamizi.
46. Kuwataarifu watu kuhusu kusudio la kufanya maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi.
47. Nyaraka zinazowasilishwa pamoja na maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi.
48. Maandalizi na yaliyomo katika mapango wa uangalizi.
49. Pale ambapo mzazi anakubali kuasiliwa.
50. Amri ya muda ya malezi au uangalizi.
51. Amri ya usimamizi.
52. Mpango wa usimamizi.
53. Mamlaka ya usmamizi.
54. Wajibu wa Msimamizi.
55. Kumtembelea motto aliye chini ya uangalizi.
56. Maombi kwa ajili ya amri ya uondoaji.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
WAJIBU WA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA KWA WATOTO WANAOHITAJI UANGALIZI

57. Wajibu kwa mtoto aliyechini ya uangalizi.
58. Wajibu wa jumla wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
59. Wajibu wa jumla wa Idara ya Ustawi wa Jamii.
60. Haki ya mzazi na wajibu chini ya amri ya uangalizi.
61. Muda wa amri ya uangalizi.
62. Kumhifadhi mtoto.
63. Kumtembelea mtoto aliye chini ya makazi ya hifadhi.
64. Kuendeshwa kwa ziara.
65. Kutoa taarifa kuhusu maoni ya eneo la makao.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

MAPITIO KUHUSIANA NA WATOTO WALIO CHINI YA UANGALIZI AU USIMAMIZI WA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MTAA


66. Mapitio.
67. Utaratibu wa mapitio ya awali.
68. Wajumbe wa mapitio.
69. Mahudhurio ya mtoto katika mkutano wa mapitio.
70. Taarifa kwa ajili ya mapitio.
71. Jukumu la mwenyekiti wa mkutano wa mapitio.
72. Kumbukumbu ya mapitio.
73. Mapitio ya pili na yatakayofuatia.
74. Mapitio ya mpango wa uangalizi kufuaitia mapitio


SEHEMU YA KUMI NA TATU

KUONDOLEWA KWA AMRI YA UANGALIZI


75. Kuondolewa kwa amri ya uangalizi.

SHERIA YA MTOTO
(SURA YA 13)

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 157(a))*

# KANUNI ZA USALAMA WA MTOTO

## SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitaitwa kama Kanuni za Usalama wa Mtoto, 2014.

Tafsiri

**2.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"malazi" maana yake ni huduma ya malazi inayotolewa mfululizo kwa kipindi kinachozidi saa ishirini na nne;

"mtoa malazi" maana yake ni mzazi wa kambo au makao yaliyothibitishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto;

Sura ya 13

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mtoto;

"mwombaji" maana yake ni mtu au kampuni iliyofanya maombi mahakamani ya shauri la madai katika Mahakama ya Watoto;

"makazi yaliyothibitishwa" maana yake ni makazi yaliyothibitishwa chini ya Sheria ya Mtoto;

"afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa" maana yake ni afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kushughulikia shauri la mtoto;

"amri ya matunzo" maana yake ni amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 18 cha Sheria;

"shauri kuhusu matunzo" maana yake ni shauri kuhusu amri ya matunzo au amri ya usimamizi chini ya kifungu cha 18 na 19 cha Sheria;

"mwangalizi" maana yake ni mtoto aliyeishi na mtu na kumpatia matunzo mtoto kwa kipindi cha angalau miezi mitatu kwa muda wa miezi sita iliyopita;

"mahakama" maana yake ni Mahakama ya Watoto iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 97 cha Sheria;

"Kamishna" maana yake ni Kamishna wa Ustawi wa Jamii;

"Idara ya Ustawi wa Jamii" maana yake ni Idara ndani ya Wizara yenye dhamana na Ustawi wa Jamii;

"kutengwa na familia" maana yake ni mtoto asiyelelewa na wazazi kutokana na wazazi wao kuwafukuza nyumbani au wanaoishi kwa namna ambayo mtoto anakosa namna nyingine zaidi ya kuondoka;

"mtu wa kuaminika" maana yake ni mtu mzima muadilifu na mwenye akili timamu ambaye si ndugu wa mtoto, na anaweza kuwa mlezi wa kambo au familia ya kambo yenye uwezo wa kumtunza mtoto iliyoidhinishwa na afisa ustawi wa jamii kuwa ina uwezo wa kumlea mtoto;

"taasisi ya kuaminika" inajumuisha makao yaliyothibitishwa au taasisi nyingine ilyoidhinishwa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii kumlea mtoto lakini haijumuishi mahabusu ya watoto, shule ya maadilisho na Magereza;

"mzazi wa kambo" au "familia ya kambo" maana yake ni mtu au familia iliyoainishwa kwenye Kanuni za Malezi ya Kambo;

"mlezi" maana yake ni mtu mwenye mamlaka au uwezo juu ya mtoto au mtu aliyeteuliwa kwa kiapo, wosia au amri ya mahakama kuchukua jukumu la malezi na usimamizi wa mali na haki za mtoto;

"Mlezi aliyeteuliwa na mahakama" maana yake ni mtu anayechukua jukumu, au aliyeteuliwa na Mahakama ya Watoto kulinda maslahi ya mtoto na kumwakilisha mtoto mahakamani;

"anayehitaji matunzo na ulinzi wa haraka" maana yake ni uwepo wa sababu za msingi zinazoonyesha kwamba mtoto yupo kwenye hatari ya kudhurika endapo hataondolewa mahali alipo;

"afisa wa ustawi wa jamii anayepokea shauri" maana yake ni afisa ustawi wa jamii mwenye wajibu wa kupokea rufaa na kuchukua hatua za dharura kwa ajili ya mtoto anayehitaji ulinzi;

"Mamlaka ya Serikali ya Mitaa" ina maana kama ilivyo kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"mtoto aliyepotea au aliyetelekezwa" maana yake ni mtoto ambaye, kutokana na maamuzi ya wazazi au sababu nyingine yoyote, hana wazazi;

"kamati ya kushughulikia watoto walio katika mazingira hatarishi" maana yake ni kamati ndogo ya kamati za

ustawi wa jamii au kamati za huduma za jamii kwenye Jiji, Manispaa, Miji na Halmashauri za Wilaya, na kwenye kata, mtaa au ngazi ya kijiji;

"amri" maana yake ni hati, wito au taratibu nyingine za mapitio au uthibitisho na maamuzi mengine ya mahakama;

"rafiki wa karibu" maana yake ni mtu anayemsaidia mtoto kufungua shauri mahakamani na inajumuisha mlezi aliyeteuliwa na mahakama;

"mzazi" maana yake ni baba au mama na baba au mama muasili wa mtoto;

"jukumu na wajibu wa mzazi" maana yake ni haki zote na wajibu ambao mzazi anao katika sheria za nchi na sheria za kimila ikijumuisha haki na wajibu ulioainishwa chini ya kifungu cha 9(3) cha Sheria;

"haki ya ulezi" kuhusiana na mtoto, maana yake ni haki na wajibu uliorejewa katika vifungu vya 6 mpaka 10 na kifungu cha 57 cha Sheria;

"mahali salama" maana yake ni mahali ambapo malezi ya mtoto chini ya ndugu, mtu anayeamikika, malezi ya kambo, taasisi inayoaminika au sehemu nyingine yoyote ambayo mtoto anaweza kukaa kwa usalama akisubiri maamuzi kutoka kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii au Mahakama ya Watoto kuhusu malezi ya baadaye, lakini haijumuishi sehemu yoyote ya kizuizi haitajumuisha mahabusi ya polisi, mahabusi ya watoto, shule ya maadilisho au jela;

"polisi" maana yake ni afisa wa polisi mwenye cheo cha konstebo;

"mwenendo wa shauri" inajumuisha maombi yoyote, rejea, shauri, usikilizwaji wa shauri, shtaka, rufaa, mapitio aidha ya kati au ya mwisho baina ya wahusika kuhusiana na mtoto;

"mtaalam" maana yake ni mwalimu, daktari mwanasaikolojia mshauri, afisa Ustawi Jamii muuguzi au mtumishi anayelea watoto ambaye anafanya kazi na au anayetoa huduma kwa mtoto anayehitaji malezi na usalama;

"sababu ya msingi ya kuamini" maana yake ni kiwango cha uthibitisho ambacho kinaweza kumfanya mtu wa kawaida kuamini kwamba ushahidi ni wa kuaminika;

"mwakilishi" maana yake ni mzazi, mlezi au mlezi aliyeteuliwa na mahakama anayemsaidia mtoto kwenye shauri

mahakamani;

"ndugu" maana yake ni babu, bibi, kaka, dada, jamaa, mjomba, shangazi au ndugu yeyote wa familia mtandao;

"uchunguzi wa kijamii; maana yake ni uchunguzi unaofanywa na Idara ya Ustawi wa Jamii;

"ripoti ya uchunguzi wa kijamii" maana yake ni taarifa ya maandishi inayoandaliwa baada ya kukamilika kwa uchunguzi wa kijamii;

"Idara ya Ustawi wa Jamii" maana yake ni idara, kitengo, chombo kingine cha kiutawala kwenye Mamlaka ya Serikali ya Mtaa inayohusika na huduma za usalama wa mtoto na inayotenda kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali ya Mtaa kulinda na kuboresha ustawi wa watoto;

"afisa ustawi wa jamii" maana yake ni afisa ustawi wa jamii aliye katika utumishi wa Serikali na inajumuisha afisa ustawi msaidizi;

"amri ya usimamizi" maana yake ni amri iliyotolewa chini ya kifungu cha 19 cha sheria; na

"malezi ya hiyari" maana yake ni kumweka mtoto kwenye malezi ya mamlaka ya serikali ya mtaa kwa ridhaa ya mzazi.

## SEHEMU YA PILI
### KANUNI ZA MSINGI YA JUMLA NA VIWANGO

Kanuni za msingi

**3.-**(1) Katika kufikia maamuzi yoyote yanayomhusu mtoto, taasisi za ustawi wa jamii, mahakama, mamlaka za serikali za mitaa, polisi, wajumbe wa Kamati ya Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi (MVCC) au chombo chochote chenye mamlaka hayo vitaongozwa na misingi ifuatayo -

(a) kipaumbele cha kwanza kitakuwa ni maslahi bora ya mtoto;

(b) mtoto anayeweza kutoa maoni apewe haki ya kutoa maoni hayo kwa uhuru kuhusu mambo yote yanayomuathiri na maoni hayo yapewe uzito stahiki kwa kuzingatia umri wake na ukomavu;

(c) mtoto anapatiwa fursa ya kusikilizwa katika shauri lolote la kimahakama linalomhusu, aidha yeye mwenyewe au kupitia mwakilishi wake au chombo stahiki, kwa mujibu wa Kanuni za Mahakama ya

watoto na Mahakama nyingine inayohusika.

(2) Pale ambapo mtoto -

(a) anapotea;

(b) anapotelekezwa au anapohitaji hifadhi;

(c) anapolelewa na Serikali ya Mtaa;

(d) anapodhurika ama kutaka kudhurika na hawezi kuishi na wazazi;

maamuzi yoyote kuhusu malezi ya mtoto yatazingatia misingi ifuatayo -

(a) kipaumbele kitakuwa ni kwa mtoto kuishi kwenye familia na si kwenye taasisi;

(b) kipaumbele kitakuwa ni kwa mtoto kuishi sehemu ya kudumu na si sehemu ya muda;

(c) isipokuwa kama ni kwa maslahi bora ya mtoto, watoto ambao ni ndugu wasitenganishwe;

(d) angalizo litakalozingatiwa ni kwa mtoto kuendelea na malezi bora, kabila la mtoto, dini, mila na lugha yake ya asili; na

(e) uchelewaji wa kufanya maamuzi kuhusu maisha ya baadaye ya mtoto utaepukwa kwani unaweza kuathiri maslahi ya mtoto.

Mtoto anayehitaji ulinzi

**4.-**(1) Mtoto atachukuliwa kuwa anahitaji malezi bora na ulinzi endapo mtoto amedhurika au yupo katika hatari ya kudhurika kwa kuzingatia moja au zaidi ya mazingira yaliyotajwa kwenye kifungu cha 16 cha Sheria, au kwa mtoto kushindwa kupata malezi kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 44 cha Sheria.

(2) Katika kanuni hii -

"madhara" maana yake ni kutendewa vibaya au kudhurika kiafya au kimaendeleo ikiwemo madhara yanayotokana na kuona au kusikia wakati mtu mwingine anatendewa vibaya;

"maendeleo" maana yake ni kukua kimwili, kiakili, kimwenendo, kijamii au kitabia;

"afya" maana yake ni afya ya mwili au ya akili;

"kutendewa vibaya" kunajumuisha udhalilishaji wa kimwili, udhalilishaji wa kijinsia na kutendewa vibaya ambazo siyo za kimwili.

(3) Madhara yanaweza kusababishwa kimwili, kihisia, udhalilishaji wa kijinsia na kutelekezwa.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3), uthibitisho kwamba madhara yametokea utajitosheleza endapo -

(a) kuna udhalilishaji wa kimwili kwa kupiga, kutikisa, kurusha, kupewa sumu au kumliza mtoto;

(b) kuna udhalilishaji wa kihisia unaotokana na mtoto kutendewa vibaya kwa muda mrefu na kupelekea madhara makubwa na ya muda mrefu na maendeleo ya mtoto, na ikijumuisha -

(i) mtoto kusikia watu wengine wakitendewa vibaya;

(ii) kuwaonyesha watoto kuwa hawana thamani au hawapendwi;

(iii) kumthamini mtoto pale tu anapotimiza mahitaji ya mtu mwingine;

(iv) matarajio yasiyo sahihi ya ukuaji wa mtoto kiumri na kimaendeleo kunakomfanya mtoto kila mara kujiona anatishiwa amani au yupo kwenye hatari;

(v) kumnyonya au kumrubuni mtoto;

(c) udhalilishaji wa kijinsia maana yake ni kumlazimisha au kumshawishi mtoto ashiriki katika shughuli za kingono, aidha kama mtoto anaelewa kinachotendeka au la na inajumuisha kugusana kimwili au kumshirikisha mtoto katika kuangalia au kuandaa picha za ngono, kuangalia mambo ya kingono, kumshawishi mtoto afanye matendo yaliyo kinyume na maadili, kutomasana kimahaba, kubakwa au kumlea mtoto kwa kumuandaa kwa ajili ya udhalilishaji;

(d) mtoto anatelekezwa kwa kushindwa kupatiwa mahitaji muhimu ya kimwili na kisaikolojia ambayo yanaweza kusababisha madhara makubwa ya kiafya au kimaendeleo kwa mtoto yakijumuisha-

(i) kushindwa kumpatia mtoto chakula cha kutosha, mavazi na malazi;

(ii) kumtelekeza na kumtenga mtoto asikae nyumbani;

(iii) kushindwa kumlinda mtoto dhidi ya

hatari zinazoweza kumsababishia madhara ya kimwili, kijinsia au kihisia;

(iv) kushindwa kumpatia mtoto huduma ya afya na matibabu; na

(v) kushindwa kumsimamia mtoto na kumpatia malezi stahiki.

(5) Katika kutathmini endapo mtoto amepata madhara, vigezo vifuatavyo vitazingatiwa -

(a) aina ya madhara endapo mtoto ametendewa visivyo, amedhalilishwa au hajapatiwa malezi stahiki;

(b) madhara kwa afya ya mtoto na maendeleo yake;

(c) maendeleo ya mtoto katika familia yake na kwenye jamii kwa ujumla;

(d) mahitaji yoyote maalum kama vile hali ya kiafya au ulemavu unaoweza kuathiri maendeleo ya mtoto na malezi katika familia; na

(e) uwezo wa wazazi na walezi wa kumlinda mtoto na kumtimizia mahitaji yake.

Vigezo vya ulinzi wa mtoto

**5.-**(1) Kamishna ataandaa vigezo vitakavyofuatwa na wakala, idara, makao au makazi yalizoidhinishwa, asasi za kiraia, watu binafsi wanaoshughulika na waliopata madhara au walioko kwenye hatari ya kupata madhara.

(2) Kamishna anaweza kuandaa kanuni za maadili kuhusu kutoa taarifa za mtoto na uwakilishi wa mtoto kwenye mikutano na waandishi wa habari na katika vyombo vingine vya habari.

## SEHEMU YA TATU

### MAJUKUMU YA JUMLA YA IDARA YA USTAWI WA JAMII

Kuanzishwa kwa idara ya ustawi wa jamii

**6.-**(1) Kila Mamlaka ya Serikali ya Mtaa -

(a) itaanzisha Idara ya Ustawi wa Jamii ya wilaya itakayosimamia na kukuza ustawi wa watoto wanaohitaji malezi na usalama;

(b) itamteua mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atakayesimamia usalama wa watoto kwenye wilaya;

(c) itahakikisha wanateuliwa maafisa ustawi wa jamii wanaotosheleza, angalu wanne katika ngazi ya wilaya watakaosimamia utoaji bora wa huduma kwa watoto wanaohitaji ulinzi; na

(d) atahakikisha kuwa angalao afisa ustawi wa jamii msaidizi atakayesimamia utoaji wa huduma kwa watoto wanaohitaji ulinzi anateuliwa katika kila kata ya wilaya husika.

(2) Mamlaka ya Serikali ya Mtaa itakasimu mamlaka yake kuhusu maslahi ya watoto kwa idara ya ustawi wa jamii.

Majukumu ya mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii

**7.-**(1) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii katika kila wilaya atahakikisha kwamba hatua zote muhimu zinachukuliwa kwa ajili kuwalinda watoto ndani ya wilaya dhidi ya aina zote za madhara zilizizoainishwa katika kanuni ya 4.

(2) Katika kutekeleza wajibu ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (1), Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii -

(a) atalinda na kukuza maslahi ya watoto wanaohitaji malezi na ulinzi katika wilaya;

(b) atahamasisha watoto kulelewa na familia zao;

(c) atachunguza na kufanya tathmini ya mazingira ya watoto wanaohitaji ulinzi;

(d) atachukua hatua stahiki kuwalinda watoto wanaoteseka au walio katika hatari ya kudhurika;

(e) ataendeleza upatikanaji wa huduma stahiki kwa watoto wanaohitaji ulinzi, ikijumuisha huduma za kifamilia zinazotolewa na jamii, huduma zinazowezesha kuchukua tahadhari, huduma za utengamao na kuchangamana, huduma za ushauri nasaha na huduma za kusaidia familia, huduma za dharura na msaada kwa watoto waliokinzana na sheria;

(f) ataainisha na ataendeleza huduma za malezi ya kambo, uandikishaji, utoaji wa mafunzo na ufuatiliaji wa wazazi au familia za kambo kwa mujibu wa Kanuni za Malezi ya Kambo, 2012;

Ts.Na.153 la 2012

(g) itaanazisha na kuendeleza huduma za kuasili na kuratibu uandikishaji na utoaji wa mafunzo kwa wazazi wanaoasili kwa mujibu wa Kanuni za Kuasili Watoto, 2014;

(h) atahakikisha malezi mbadala ya familia yanapatikana yakijumuisha malezi ya kambo, makao na taasisi zilizothibitishwa ili kukidhi mahitaji ya watoto waliokosa malezi ya familia kwa mujibu wa Kanuni za Makao ya Watoto na Kanuni za Malezi ya Kambo;

(i) ataanzisha na kutunza rejesta ya watoto walio katika mazingira hatarishi katika eneo lake;

(j) ataazisha na kutunza rejesta ya watu wasiofaa kufanya kazi na watoto;

(k) atapunguza makosa ya jinai yanayotendwa na watoto kwa utaratibu endelevu wa -

- (i) huduma za kuchukua tahadhari kwa watoto;
- (ii) huduma za ushauri na kuwasaidia wazazi katika kufuatilia tabia za watoto wao;
- (iii) huduma za malazi kwa watoto ambazo walipaswa kuwekwa kizuizini kabla na baada ya kesi zao kusikilizwa;
- (iv) huduma za kuwasaidia watoto kuchangamana na familia zao na jamii baada ya kutenda makosa, na kupunguza uwezekano wa kurudia kutenda makosa.

(l) atawajibika kuripoti kwa Mkurugenzi wa Wilaya;

(m) ataandaa mpango wa usalama wa mtoto wa mwaka ambao utakuwa ni sehemu ya Mkakati wa Matumizi ya Muhula wa Kati (MTEF);

(n) atatoa ripoti kila mwaka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kuhusu utekelezaji wa mpango wa usalama wa mtoto; na

(o) atatekeleza Kanuni zote na viwango vya ubora vitakavyotolewa na Kamishna.

(3) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii ataingia kwenye makubaliano na Asazi Zisizo za Kiserikali (AZISE) zilizosajiliwa kwa ajili ya kutoa huduma zilizorejewa kwenye kifungu kidogo cha (2)(e)(h) na (k).

(4) Asasi yoyote ya kiraia inayofanya kazi chini ya makubaliano, mkataba au msaada wa kutoa huduma kwa

watoto chini ya kifungu kidogo cha (2)(e) – (h) na (k) itawajibika kutimiza vigezo vyote vya ubora vitakavyotolewa na Kamishna.

Kukuza uelewa wa jamii

**8.-**(1) Mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atakuwa na jukumu la kukuza uelewa kuhusu usalama wa mtoto kwenye jamii, ikijumuisha taarifa kuhusu namna ya kuwasilisha suala linalohusu usalama wa mtoto.

(2) Katika kukuza uelewa, mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atahakikisha kwamba taarifa zinazoendana na umri wa mtoto zinatolewa moja kwa moja kwa mtoto kwa njia ya maandishi au kwa njia nyingine.

Maelezo kwa wanataaluma

**9.-**(1) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii atawajibika kuwaelewesha wataalam, watumishi na watoa huduma wanaohusika na watoto na familia namna ya kuwasilisha suala linalohusu usalama wa mtoto, ikijumuisha jina la mtu au afisa ambaye suala hilo litawasilishwa kwake, namba ya simu na namna nyingine ya mawasiliano itakayoweza kutumiwa.

(2) Taarifa inaweza kuwasilishwa kwa maandishi au kwa njia nyingine yoyote.

## SEHEMU YA NNE
### RAFAA KUHUSU USALAMA WA MTOTO

Afisa mapokezi wa ustawi wa jamii

**10.** Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii atahakikisha kwamba afisa mapokezi wa ustawi wa jamii anakuwepo muda wote ili kupokea rufaa kuhusu usalama wa mtoto.

Rufaa ya mtoto iliyoletwa na mwanajamii

**11.-**(1) Mwanajamii yeyote ambaye ana sababu ya msingi ya kuamini kwamba -

(a) mtoto anadhurika au yupo kwenye hatari ya kupata madhara kwa namna iliyo kwenye kanuni ya 4;
(b) mtoto amepotea, ameteketezwa au ametengwa na nyumbani kwake;
(c) mtoto anashughulishwa katika ajira mbaya;
(d) mzazi, mlezi, ndugu au mwangalizi hampatii mtoto chakula, malazi haki ya kucheza na kufurahi,

mavazi, matibabu au elimu,

atatoa taarifa ya suala hilo kwa mamlaka ya serikali ya eneo husika.

(2) Rufaa kuhusu usalama wa mtoto inaweza kutolewa na mwanajamii kwa mdomo au kwa maandishi au kwa kupiga simu kwenye idara inayohusika na watoto.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka ya Serikali ya Mtaa itajumuisha -

(a) afisa wa ustawi wa jamii wa wilaya;
(b) afisa ustawi wa jamii wa kata;
(c) afisa ustawi wa jamii wa wilaya;
(d) Afisa Mtendaji wa Kata;
(e) mwenyekiti wa kijiji au mwenyekiti wa mtaa;
(f) mjumbe wa Kamati ya Kuhudumia Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi;
(g) afisa wa polisi wa eneo husika.

(4) Pale ambapo taarifa inawasilishwa kwa mmoja wa watu walioorodheshwa kwenye kanuni ndogo ya (3)(c), (d), (e), (f) na (g), mtu huyo ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu alipopokea taarifa hiyo, atamtaarifu afisa ustawi wa jamii kwenye kata hiyo au afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri.

(5) Pale ambapo afisa ustawi wa jamii wa kata au afisa ustawi wa jamii wa wilaya atakapopewa taarifa, atamtaarifu afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri ndani ya saa ishirini na nne (24) baada ya kupokea taarifa hiyo.

(6) Afisa mapokezi wa ustawi wa jamii, ndani ya saa ishirini na nne (24) baada ya kupokea taarifa, ataitathmini taarifa hiyo na kufanya maamuzi endapo ni ya msingi na endapo inahitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi.

(7) Taarifa za mtoa taarifa zitafanywa kuwa siri na watu wote walioorodheshwa kwenye kanuni ndogo ya (3) na isipokuwa kwa ruhusa ya Mahakama ya Watoto, hazitatolewa kwa mtu yeyote isipokuwa kwa watu waliotajwa kwenye kanuni ndogo ya (4).

(8) Afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri ndani ya saa sabini na mbili (72) toka alipopokea taarifa kutoka kwa mwanajamii au kwa mtu aliyeorodheshwa kwenye kanuni ndogo ya (3), pale itakapowezekana, atamtaarifu mtoa taarifa kwamba taarifa imepokelewa na itafanyiwa kazi.

Rufaa ya mtoto kutoka kwa mtaalam

**12.-**(1) Mtaalam yeyote, mtumishi au mtu anayejitolea kufanya kazi au kutoa huduma kwa watoto au familia, ambaye ana sababu za msingi za kuamini kwamba -

(a) mtoto anadhurika au yupo kwenye hatari ya kupata madhara kwa namna iliyo kwenye kanuni ya 4;

(b) mtoto amepotea ametelekezwa au ametengwa na nyumbani kwake;

(c) mtoto anashughulishwa katika ajira ya mbaya;

(d) mzazi, mlezi, ndugu au mwangalizi hampatii mtoto chakula, malazi, haki ya kucheza na kufurahi, mavazi, matibabu au elimu,

atawasilisha suala hilo kwa afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri au kwa afisa ustawi wa jamii katika kata inayohusika na usalama wa mtoto huyo.

(2) Kupokelewa kwa rufaa kutathibitishwa kwa maandishi na nakala yake itahifadhiwa kwa kumbukumbu.

(3) Pale ambapo rufaa inawasilishwa kwa afisa ustawi wa jamii kwenye kata, afisa huyo atamtaaarifu afisa mapokezi wa ustawi wa jamii ndani ya saa ishirini na nne (24) baada ya kupokea taarifa hiyo.

(4) Mtu yeyote anayetoa taarifa chini ya kanuni hii, ataifanya taarifa hiyo kuhusu mtoto kuwa ya siri na hataitoa taarifa hiyo kwa mtu mwingine isipokuwa kwa -

(a) afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri au afisa ustawi wa jamii wa kata husika au kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii;

(b) afisa wa polisi endapo kuna sababu ya kuamini kuwa kosa limetendwa dhidi ya mtoto;

(c) mkutano wa usalama wa mtoto; au

(d) mahakamani wakati wa kutoa ushahidi kwenye kosa lililotendwa dhidi ya mtoto au kwenye shauri la madai kuhusiana na malezi na usalama wa mtoto.

Utaratibu baada ya kupokelewa kwa rufaa za usalama wa mtoto

**13.-**(1) Baada ya kupokea rufaa chini ya kanuni za 11 au 12, afisa mapokezi wa ustawi wa jamii -

(a) atajiridhisha endapo kuna taarifa kuhusu mtoto huyo zilizokwishatolewa hapa awali; na

(b) endapo faili la mtoto huyo lilishafunguliwa.

(2) Endapo faili kuhusiana na mtoto huyo lilishafunguliwa na kufungwa, litafunguliwa tena.

(3) Pale ambapo hakuna taarifa za mtoto huyo zilizokwishatolewa hapo awali, faili lenye jina la mtoto huyo litafunguliwa.

(4) Kufunguliwa kwa faili la mtoto huyo hakutazuia kurekodiwa kwa taarifa hizo kwa njia ya kielektroniki kwa mujibu wa uratibu wa mashauri uliopo.

(5) Kila faili la mtoto litajumuisha -

(a) tarehe ya rufaa;

(b) jina la mtoa taarifa, endapo linafahamika;

(c) endapo mtoa taarifa ni mwanajamii au ni mtaalam, mtumishi au mtu anayefanya kazi kwa kujitolea;

(d) jambo liloelezwa;

(e) taarifa za msingi za mtoto, zikijumuisha jina la mtoto, umri, anuani, majina ya wazazi, mlezi au mwangalizi, shule au kituo anachohudhuria na endapo mtoto ana ndugu.

(6) Endapo baada ya kupokea taarifa, afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri atakuwa na sababu za kuamini kuwa mtoto husika hayupo kwenye hatari ya kudhurika, afisa mapokezi wa ustawi wa jamii anaweza kumwomba afisa ustawi wa jamii wa kata kupata ufafanuzi kutoka kwa mtoa rufaa, ikijumuisha rufaa zinazotolewa na familia, apate asili ya malalamiko kwa namna gani na kwanini limeibuka.

(7) Pale ambapo maombi yatakapofanywa chini ya kanuni ndogo ya (6), taarifa inapaswa kumfikia mhusika ndani ya saa arobaini na nane (48).

(8) Afisa ustawi wa jamii kwenye kata anaweza kupata taarifa husika kwa kukutana na mtoa taarifa au kwa kutumia njia nyingine ya mawasiliano ikijumuisha simu na barua pepe.

(9) Afisa ustawi wa jamii atampatia afisa mapokezi wa ustawi wa jamii aneyepokea rufaa yoyote iliyopatikana ndani ya saa ishirini na nne (24) baada ya kupata taarifa hiyo.

(10) Baada ya kupokea taarifa chini ya kanuni ndogo ya (9), afisa ustawi wa jamii anayepokea rufaa atatathmini endapo suala husika ni la msingi na endapo uchunguzi ufanyike ndani ya saa ishini na nne.

(11) Endapo itaamuliwa kwamba uchunguzi wa awali usifanyike, afisa mapokezi wa ustawi wa jamii anayepokea

rufaa-

(a) atamtaarifu mtaalam, mfanyakazi au mtoa huduma ndani ya saa ishirini na nne (24) baada ya maamuzi yanayomtaka asiendelee na uchunguzi;
(b) atayanakili maamuzi hayo kwenye faili la mtoto pamoja na sababu za kufikia maamuzi hayo; na
(c) endapo hapatakuwa na hatua nyingine za kuchukua, atalifunga faili.

## SEHEMU YA TANO
### UCHUNGUZI WA AWALI

Kufanya uchunguzi wa awali

**14.**-(1) Endapo afisa ustawi wa jamii anayepokea ushauri-

(a) baada ya kupokea rufaa kuhusu usalama wa mtoto kwa mujibu wa kanuni za 11 na 12 ana sababu ya msingi na atahitimisha kwamba uchunguzi ufanyike;
(b) atakapopokea rufaa husika au rufaa kutoka polisi;
(c) atakapopokea rufaa ya usalama wa mtoto kutoka mahakama ya watoto;
(d) atapewa taarifa na mzazi, mlezi au mtu yeyote mweye jukumu la kumlea mtoto kwamba hawezi tena kumlea mtoto huyo; au
(e) ana sababu za kuamini kuwa mtoto aliye kwenye wilaya yake anahitaji ulinzi kwa mujibu wa kanuni ya 4 na kifungu cha 16 cha Sheria,

Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii ataelekeza uchunguzi wa awali ufanyika ili kubainisha endapo pana hoja ya kuingilia kati ili kuhakikisha kwamba mtoto hadhuriki au haendelei kuwa katika hatari ya kudhurika.

(2) Afisa Ustawi Jamii anayepokea mashauri atafanya uchunguzi wa awali au mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii atamteua -

(a) afisa kutoka idara ya ustawi wa jamii;
(b) afisa ustawi wa jamii kwenye kata; au
(c) endapo hakuna afisa ustawi wa jamii kwenye kata na kuna upungufu wa watumishi katika idara ya ustawi wa jamii, mjumbe wa kamati ya watoto

walio katika mazingira hatarishi wa kata aliyepata mafunzo atafanya uchunguzi wa awali.

(3) Maombi yatafanywa kwa mujibu wa aya ya 2(c) kwa mjumbe wa kamati ya watoto walio katika mazingira hatarishi aliyepata mafunzo ya kufanya uchunguzi kuhusu usalama wa mtoto.

(4) Uchunguzi wa awali utafanywa kwa mujibu wa miongozo itakayotolewa na Kamishna.

(5) Afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri au mtu aliyeteuliwa chini ya kanuni ndogo ya (2) atahakikisha kwamba -

(a) kwa taarifa zinazowasilishwa chini ya aya za (1)(a), (b) ,(c), (d) na (e), taarifa inayotolewa inathibitishwa kupokelewa ndani ya saa sabini na mbili (72);

(b) pale ambapo kuna ushahidi kwamba mtoto yupo katika hatari ya kudhurika au nguvu za dharura zimetumika chini ya Kifungu cha 96(2) cha Sheria, uchunguzi wa awali ulifanywa na afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri, umekamilika ndani ya saa ishirini na nne(24); na

(c) katika matukio yoyote mengine, uchunguzi wa awali umeanza ndani ya saa sabini na mbili (72) na unatakiwa kukamilika ndani ya siku saba.

(6) Taarifa ya maandishi kuhusu uchunguzi wa awali itawekwa kwenye faili la mtoto.

Uchunguzi wa awali unaofanywa kwa pamoja na Polisi

**15.-**(1) Pale ambapo taarifa iliyopokelewa na idara ya ustawi wa jamii inajumuisha kosa la jinai lililotendwa dhidi ya mtoto, afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri atajadili suala hilo na polisi mapema iwezekanavyo kabla ya kupita saa ishirini na nne (24) baada ya taarifa kutolewa.

(2) Afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri kwa kushirikiana na polisi atatathmini -

(a) ni namna gani uchunguzi utafanyika;

(b) ni namna gani familia na mtu yeyote aliyetuhumiwa atakavyohojiwa;

(c) mtu sahihi wa kufanya mahojiano;

(d) endapo mtoto anapaswa kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu;

(e) mtu sahihi wa kumhoji mtoto ambaye anahusika na taarifa zilizowasilishwa;

(f) mtu sahihi wa kumhoji mtoto mwingine yeyote kwenye familia au mtoto mwingine yeyote aliyekutwa kwenye mazingira ambapo afisa ustawi wa jamii au afisa wa polisi ana sababu ya kuamini kuwa anaweza akawa amedhurika au yupo kwenye hatari ya kupata madhara;

(g) mambo yatakayohojiwa;

(h) namna mahojiano yatakavyorekodiwa.

Kumhoji mtoto wakati wa uchunguzi

**16.-**(1) Afisa ustawi wa jamii atahakikisha kwamba, wakati wa kufanya uchunguzi, mtoto anayeweza kujieleza mwenyewe anajieleza peke yake pasipo uwepo wa mzazi.

(2) Madhumuni ya mtoto kujieleza mwenyewe ni kutathmini endapo kuna sababu za msingi za kuamini kwamba mtoto amedhurika au yupo kwenye hatari ya kupata madhara.

(3) Pale ambapo kuna sababu za msingi za kuamini kwamba kosa la jinai limetendwa dhidi ya mtoto, na mahojiano na mtoto ni muhimu kufanyika ili kukusanya ushahidi, afisa wa polisi atamhoji mtoto mbele ya afisa ustawi wa jamii.

(4) Mtoto atahojiwa na afisa ustawi wa jamii au afisa wa polisi aliyepata mafunzo ya kitaalam ya kuwahoji watoto waliopata madhara au walio katika hatari ya kupata madhara au wahanga au mashuhuda wa uhalifu.

(5) Mtoto hatahojiwa mbele ya mtu yeyote anayetuhumiwa kumdhalilisha mtoto au anayetuhumiwa kula njama na mtu aliyemdhalilisha mtoto.

(6) Pale ambapo afisa ustawi wa jamii ataona ni lazima, mtoto atafanyiwa uchunguzi wa kitabibu.

(7) Mahojiano yanaweza kuahirishwa ili kuwezesha mtoto kufanyiwa uchunguzi wa Kitabibu, lakini mahojiano hayo yataendelea mara tu baada ya uchunguzi, isipokuwa kama si kwa maslahi ya mtoto.

(8) Mahojiano na mtoto yatakuwa ya muda mfupi na kwa lengo hili, pale itakapowezekana, yatarekodiwa kwa njia ya kusikia na ya kuona.

(9) Endapo mtoto haelewi lugha ya majadiliano, atapatiwa mkalimani bila malipo.

Kukubalika kwa ushaidi wa kusikia na kuona

**17.-**(1) Tepu yoyote ya kusikia au ya kuona iliyotengenezwa wakati wa kumhoji mtoto, itakubalika katika shauri lolote la jinai pale mtu anaposhtakiwa kwa kutenda kosa dhidi ya mtoto au katika shauri lolote linalohusu usalama wa mtoto na inaweza kutumika yote au sehemu yake kama ushahidi wa mtoto katika shauri la jinai.

(2) Tepu ya maneno au ya sauti iliyohaririwa haitakubalika mahakamani kama ushahidi.

(3) Tepu za maneno na za sauti zitaandaliwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa mwongozo utakaotolewa na Kamishna.

Kushindwa kumfanya mtoto apatikane wakati wa uchunguzi

**18.** Pale ambapo–

(a) panapokuwa na sababu ya msingi ya kuamini kuwa mtoto anadhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika;

(b) mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ameelekeza uchunguzi wa awali ufanyike kwa mujibu wa kanuni ya (14); na

(c) wazazi, mlezi au mwangalizi hawataki kushiriki au kufanya mtoto apatikane kwa ajili uchunguzi unaofanywa na afisa ustawi wa jamii au afisa wa polisi,

afisa ustawi wa jamii akiongozana na afisa wa polisi, kwa mujibu wa kifungu cha 9(1) cha Sheria, wanaweza kuingia na kufanya upekuzi katika eneo lolote ambalo mtoto huwa anaishi au eneo ambalo wanaamini mtoto amewekwa kwa lengo la kupeleleza, na pale ambapo afisa ustawi wa jamii atakapoamini kuwa mtoto amedhalilishwa au anahitaji matunzo ya ulinzi kwa haraka, anaweza kumwondoa mtoto huyo au mtoto mwingine yeyote katika eneo hilo na kumweka sehemu yenye usalama kwa mujibu wa kanuni ya 22.

Amri ya kutafuta na kuonyesha

**19.-**(1) Pale ambapo mazingira yaliyotajwa katika Kanuni ya 18(1)(a), (b) na (c) yanapotokea, na afisa ustawi wa jamii na afisa wa polisi wanashindwa kumpata mtoto, maombi ya dharura yanaweza kufanywa mahakamani na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali ya Mtaa ili kupata amri ya ulinzi ya dharura au amri ya usimamizi na katika maombi hayo anaweza kuomba mahakama itoe amri ya kutafuta na kuonyesha kwa mujibu wa Sehemu ya Kumi na Ne

Ts. Na.251 la 2014

ya Kanuni za Mahakama ya Watoto.

(2) Maombi yatafanywa kwa mujibu wa kanuni ya 140(2) ya Kanuni za Mahakama ya Watoto.

(3) Pale ambapo mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ana sababu za kuamini kuwa mzazi, mlezi au mwangalizi ambaye kwaye amri ya kutafuta na ya kuonyesha imetolewa, anaweza kumtoa mtoto kutoka katika eneo ambalo inaaminika kuwa mtoto yupo na anaweza kupeleka maombi ya upande mmoja mahakamani kuomba amri ya kutafuta na ya kuonyesha kwa niaba ya mamlaka ya serikali ya mtaa kwa mujibu wa kanuni ya 142(1) ya Kanuni za Mahakama ya Watoto.

TS. Na 251 la 2014

(4) Mahakama inapotoa amri ya kutafuta na ya kuonyesha -

(a) inaweza kumpa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa mamlaka ya serikali ya mtaa amri ya kuingia kwenye eneo lililotajwa na kumwondoa mtoto huyo au mtoto mwingine atakayekutwa kwenye eneo hilo na kumweka katika sehemu salama pale patakapokuwa na sababu ya msingi ya kuamini kuwa mtoto huyo anadhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika;

(b) inaweza kumtaka mzazi au mlezi kumpeleka mtoto katika sehemu na muda utakaoamuliwa na mahakama.

(5) Endapo ambapo mahakama imetoa amri ya upande mmoja, amri hiyo inaweza kutekelezwa, ila mzazi, mlezi au mtoa matunzo ataonyeshwa amri hiyo wakati afisa ustawi wa jamii atakapoingia kwenye eneo hilo.

(6) Pale ambapo amri ya upande mmoja inapotolewa, wazazi, mlezi au mwangalizi watakuwa na haki ya kufanya maombi ya kuitengua amri hiyo ya upande mmoja ya kutafuta na ya kuonyesha kwenye Mahakama ya Watoto ndani ya saa sabini na mbili (72) toka amri hiyo ilipotolewa.

(7) Mamlaka ya Serikali ya Mtaa baada ya kupewa amri ya kutafuta na ya kuonyesha, inaweza kuiomba mahakama kusitisha amri hiyo ya kutafuta na kuonyesha wakati uchunguzi wa awali unafanyika.

(8) Endapo baada ya uchunguzi, Mamlaka ya Serikali ya Mtaa itaona si lazima kupata amri ya malezi na usimamizi,

inaweza kuondoa maombi ya amri ya malezi na usimamizi.

Mzazi kutoridhia uchunguzi wa kitatibu

**20.-**(1) Pale ambapo-

(a) kuna sababu za msingi za kuamini kuwa mtoto anadhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika;

(b) afisa ustawi wa jamii atakapoamua kwamba mtoto au mtoto mwingine yeyote anayeishi kwenye nyumba afanyiwe uchunguzi wa kitabibu; na

(c) wazazi, mlezi au mwangalizi anakataa kutoa ridhaa ili uchunguzi huo ufanyike,

afisa ustawi wa jamii atatafuta njia mbadala ili kupata ridhaa ya kufanya uchunguzi na namna nyingine ya matibatu ya mtoto.

(2) Pale ambapo mazingira yaliyoko kwenye kifungu kidogo cha (1) yametokea, ridhaa inaweza kutolewa na mtoto endapo ana ukomavu wa kutosha wa kuelewa ni kwanini uchunguzi wa kitabibu pamoja na matibabu mengine ya msingi yanatolewa.

(3) Tathmini endapo mtoto ana umri na ukomavu wa kutosha itafanywa na daktari anayefanya uchunguzi.

(4) Katika hali yoyote endapo matibabu ya dharura yanahitajika ili kuokoa maisha ya mtoto au kuzuia ulemavu wa kudumu kwa mtoto, daktari anaweza kuendelea na matibabu bila kupata ridhaa ya mzazi au ya mtoto.

(5) Katika hali nyingine yoyote, endapo ridhaa haiwezi kupatikana, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kwa niaba ya mamlaka ya serikali ya mtaa ataomba amri mahakamani chini ya kifungu cha 95(3)(a) cha Sheria kuruhusu uchunguzi ufanyike. Maombi hayo yatasikilizwa siku ya maombi hayo yamefanywa.

Mtoto kuridhia uchunguzi wa kitabibu

**21.-**(1) Daktari anayetaka kufanya uchunguzi wa kitabibu kwa mtoto mwenye umri na ukomavu wa kutosha atapata kwanza ridhaa kutoka kwa mtoto huyo.

(2) Pale ambapo mtoto mwenye umri na ukomavu wa kutosha anakataa kutoa ridhaa na endapo mtoto huyo asipofanyiwa uchunguzi na kutibiwa anaweza kupoteza maisha au kupata ulemavu wa kudumu, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kwa niaba ya mamlaka ya serikali ya mitaa anaweza kuomba amri mahakamani chini ya kifungu cha 95(3)(a) cha Sheria kuruhusu uchunguzi wa kitabibu na matibabu kutolewa. Maombi haya yatasikilizwa siku maombi haya yamefanywa.

## SEHEMU YA SITA
### MAHALI SALAMA

Kumweka mtoto mahali salama

**22.-**(1) Endapo afisa ustawi wa jamii ana sababu za msingi za kuamini kuwa mtoto anadhurika au anaweza kudhurika, anaweza kwa kuongozana na afisa wa polisi, kuingia na kupekua eneo alipo mtoto ili kufanya uchunguzi.

(2) Endapo baada ya kuingia na kufanya uchunguzi, afisa ustawi wa jamii atajiridhisha kwamba mtoto yupo kwenye hatari ya dhahiri ya kudhurika, afisa ustawi wa jamii kwa kuongozana na afisa wa polisi anaweza kumwondoa mtoto kutoka kwenye eneo hilo na kumweka kwenye mahali salama kwa kipindi kisichozidi siku saba.

(3) Pale ambapo afisa ustawi wa jamii atatathmini kwamba mtoto aliye hospitali au aliyepewa hifadhi na idara ya ustawi wa jamii chini ya kifungu cha 38 au anayeishi na mtoa huduma kwa muda atakuwa kwenye hatari ya kudhurika endapo ataondolewa kwenye sehemu hiyo na mzazi, mlezi au mtoa huduma, afisa ustawi wa jamii atatamka kuwa hospitali au sehemu alipo mtoto kwa muda huo ni mahali salama ili kuzuia mtoto asiondolewe.

(4) Pale ambapo mtoto atakapoondolewa kutoka kwa mzazi, mlezi au mwangalizi chini ya kanuni ndogo ya (2) na (3), afisa ustawi wa jamii atamtaarifu mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu kuondolewa.

(5) Mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atahakikisha kwamba mtoto aliyewekwa kwenye mahali ya usalama anapatiwa malazi, aidha na mzazi, mlezi wa kambo, mtu mwenye uwezo kwenye hospitali au ikishindikana kabisa, kwenye makao yaliyoidhinishwa.

(6) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, ndani ya saa sabini na mbili baada ya kupokea taarifa chini ya kauni ndogo ya (4), atamfanyia uchunguzi wa awali mtoto yeyote aliyewekwa mahali yenye usalama.

(7) Wakati mtoto yupo kwenye mahali salama, haki na majukumu ya wazazi yatatolewa kwa ushirikiano na Mamlaka ya Serikali ya Mtaa na haki hiyo na wajibu wa mzazi itakuwa kwa kiasi itakavyoamuliwa na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kwa niaba ya mamlaka ya serikali ya mtaa.

(8) Pale mtoto atakapowekwa kwenye sehemu ya

usalama na polisi pasipo uwepo wa afisa ustawi wa jamii, polisi atamtaarifu afisa mapokezi wa ustawi wa jamii mapema.

(9) Wazazi, walezi au mwangalizi wa mtoto aliyewekwa kwenye mahali usalama -

(a) watapewa taarifa mapema iwezekanavyo na watu wanoishi na mtoto, isipokuwa kama kuna sababu za msingi za kuamini kuwa kwa kufanya hivyo kutamdhuru mtoto;

(b) watapewa mawasiliano na mtoto isipokuwa kama kwa kufanya hivyo kutakuwa si kwa maslahi ya mtoto.

(10) Mzazi au mlezi anaweza kukata rufaa kwenye mahakama ya watoto na endapo mahakama ya watoto haisikilizi mashauri, atakata rufaa kwenye mahakama yenye mamlaka -

(a) kupinga afisa ustawi wa jamii kumwondoa mtoto na kupelekwa kwenye sehemu ya usalama;

(b) kupinga kunyimwa mawasiliano na mtoto.

Kuongeza muda wa kukaa kwenye sehemu ya usalama

**23.-**(1) Pale ambapo mtoto ameondolewa na kuwekwa kwenye mahali usalama chini ya kanuni ya 22(2) au (3), afisa usatawi wa jamii aliyemtoa mtoto atawasiliana na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ndani ya saa sabini na mbili baada ya mtoto kuondolewa ili kutathmini endapo maombi ya kuongeza muda wa kukaa kwenye mahali salama yafanywe kwenye mahakama ya watoto.

(2) Katika kuamua endapo maombi ya kuongeza muda yafanywe, usalama wa mtoto utapewa kipaumbele.

(3) Katika kutathmini maslahi ya mtoto, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atazingatia -

(a) sababu za kumtoa mtoto na kumweka sehemu ya usalama;

(b) sababu za afisa ustawi wa jamii kujihusisha na mtoto na familia yake hapo awali;

(c) endapo uchunguzi wa awali umehitimishwa;

(d) uwezekano kwamba mtoto atadhurika au atakuwa kwenye hatari ya kudhurika endapo atarejeshwa nyumbani kwake;

(e) maoni na matarajio ya mtoto kwa kuzingatia umri na ukomavu wake.

(4) Pale ambapo maamuzi yamefanywa ya kuomba kuongezwa muda wa kuwekwa mahali salama, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kwa niaba ya mamlaka ya serikali ya mtaa anaweza kufanya maombi mahakamani kuongeza muda wa kukaa kwenye mahali salama kwa mujibu wa Kanuni ya 117 ya Kanuni za Mahakama ya Watoto.

TS.No.251 la 2014

(5) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (4) yatafanywa ndani ya siku zisizozidi tano (5) toka mtoto alipowekwa mahali salama.

(6) Maombi ya amri ya kutoa malezi inaweza kufanywa kwa pamoja na maombi ya kuongeza muda wa kukaa kwenye sehemu yenye usalama kwa mujibu wa kanuni za 44 mpaka 38.

(7) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii atawataarifu wazazi wa mtoto kwamba mamlaka ya serikali ya mtaa ina nia ya kuomba kuongeza muda wa kuwekwa kwenye mahali salama kabla ya siku ambayo maombi yamefanywa.

(8) Idara ya Ustawi wa Jamii itafanya Uchunguzi na kuchukua hatua zinazostahili kuthibitisha utambulisho wa wazazi na makazi yao, lakini endapo utambulisho hautapatikana, idara ya ustawi wa jamii itaitaarifu mahakama ili hitaji la kuwatambua wazazi liachwe.

(9) Pale ambapo maombi ya kuongeza muda wa kuwekwa mahali salama yamekubaliwa na mahakama lakini afisa ustawi wa jamii anaona itakuwa ni salama zaidi kwa mtoto kurejeshwa kwa mzazi, mlezi au mwangalizi.

## SEHEMU YA SABA
### HATUA KUFUATIA UCHUNGUZI

Hatua kufuatia uchunguzi

**24.-**(1) Kufuatia uchunguzi, afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri kwa kushauriana na mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, na endapo kuna sababu za msingi za kuamini kuwa kosa limetendeka, ataamua kwa kushirikiana na polisi endapo -

(a) hakuna sababu ya msingi ya kuamini kwamba mtoto huyo au mtoto mwingine kwenye nyumba amedhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika-

(i) hakuna hatua nyingine inayohitaji kuchukuliwa; au

(ii) familia inapaswa kupelekwa kwenye Kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ya eneo hilo kwa ajili ya kupewa msaada; au

(b) hakuna sababu za msingi za kuamini kuwa mtoto huyo au mtoto mwingine yeyote katika nyumba anadhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika lakini familia hiyo inapaswa kupelekwa kwenye Kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ya eneo hilo kwa ajili ya kupewa msaada; au

(c) kuna sababu ya msingi ya kutia shaka**.**

(2) Pale ambapo itakapoamuliwa kwamba aya ya (1)(a) itumike, faili la mtoto litafungwa na mtoa taarifa atajulishwa.

(3) Pale ambapo mzazi au mlezi anaposhtakiwa kwa kosa la jinai kuhusiana na mtoto kutokana na matokeo ya uchunguzi wa awali, faili la mtoto halitafungwa mpaka shauri hilo la jinai dhidi ya mtu huyo atakapoipeleka litakapohitimishwa.

Kumtaarifu mrufaniwa kuhusu hatua zitakazochukuliwa

**25.-**(1) Pale ambapo afisa ustawi wa jamii anayepokea Mashauri ameamua kutochukua hatua au familia kwenye Kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kwa mujibu wa kanuni ya 24(1)(a), mrufaniwa atajulishwa kuhusu upelelezi na kwamba mtoto hajadhurika na hayupo kwenye hatari ya kudhurika, ila hatapewa taarifa kuhusu matokeo ya uchunguzi wala taarifa binafsi kuhusu familia na mtoto huyo.

(2) Pale ambapo rufaa itakapofunguliwa na mtaalam, mtumishi au mtu anayefanya kazi za watoto kwa kujitolea, na afisa ustawi wa jamii aneyepokea mashauri akaamua kutochukua hatua yoyote au kutoipeleka familia kwenye Kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, mtoa taarifa atajulishwa matokeo na maamuzi kutokana na uchunguzi kwa maandishi na nakala itawekwa kwenye faili la mtoto.

(3) Endapo Idara ya Ustawi wa Jamii itaamua kutokuchukua hatua yoyote na kulifunga faili la mtoto, faili hilo litahifadhiwa mpaka mtoto huyo atakapotimiza miaka ishirini na moja (21).

(4) Endapo afisa mapokezi wa ustawi wa jamii anayepokea mashauri ataamua kwamba kuna sababu ya kutia

shaka -

(a) mtoa taarifa ambaye ni mwanajamii atajulishwa kwamba sula lake bado linafanyiwa tathmini na kwamba atajulishwa matokeo yake baada ya uamuzi kutolewa;

(b) mtoa taarifa ambaye ni mtaalam atajulishwa kwa maandishi kwamba uchunguzi wa awali umefanyika na utafuatiwa na uchunguzi wa kijamii, na baada ya hapo atajulishwa kuhusu uamuzi uliofanywa.

Utaratibu endapo kuna cause for concern kufuatia uchunguzi

**26.-**(1) Endapo baada ya uchunguzi, afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri atahitimisha kwa mujibu wa kanuni ndogo ya 24(1) kwamba kuna sababu ya kutia shaka, uchunguzi wa kijamii utafanywa na utakamilika ndani ya siku saba.

(2) Taarifa ya uchunguzi wa kijamii itabainisha -

(a) endapo mtoto anadhurika au yupo kwenye hatua ya kudhurika;

(b) endapo mzazi, mlezi au mwangalizi ana uwezo wa kuboresha afya na maendeleo ya mtoto; na

(c) endapo mzazi, mlezi au mwangalizi anaweza kutimiza mapema mahitaji ya mtoto.

(3) Katika kufanya uchunguzi wa kijamii, afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri-

(a) endapo mtoto ana ukomavu wa kutosha, ataongea na mtoto;

(b) endapo mtoto hajafikia umri wa ukomavu, ataongea na wazazi, mlei zu mwangalizi na ndugu wa mtoto;

(c) atachukua taarifa muhimu kutoka kwa mtaalam na kutoka kwa watu wa karibu na mtoto na familia yake;

(d) endapo itahitajika, atafanya mipango ya mtoto kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu;

(e) atazingatia taarifa zote za muhimu ikijumuhisha taarifa za historia ya mtoto;

(f) atachanganua taarifa zilizopatikana kutoka vyanzo vyote ikijumuisha kumbukumbu zilizopo.

(4) Kufuatia uchunguzi wa kijamii, afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri kwa kushauriana na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii, na pale patakapokuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa kosa limetendeka, kwa kushauriana na polisi,

ataamua endapo -

(a) hakuna sababu ya msingi ya kuamini kwamba mtoto huyo au mtoto mwingine yeyote kwenye nyumba husika anadhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika na kwamba hamna hatua nyingine itakayochukuliwa;

(b) hakuna sababu ya msingi ya kuamini kwamba mtoto huyo au mtoto mwingine yeyote kwenye nyumba husika anadhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika lakini familia ipelekwe kwenye Kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ya eneo husika ili kupatiwa msaada; au

(c) kuna sababu ya msingi ya kuamini kwamba mtoto anadhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika na suala la mtoto huyo linapaswa kupelekwa kwenye kikao cha usalama wa mtoto;

(d) mtoto anadhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika na hatua za dharura zinapaswa kuchukuliwa ili kumlinda mtoto.

(5) Endapo itaamuliwa kwamba hatua za dharura zinapaswa kuchukuliwa, afisa ustawi wa jamii, baada ya kushauriana na mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, anaweza kumwondoa mtoto na kumweka kwenye mahali salama kwea mujibu wa kanuni ya 22.

## SEHEMU YA NANE
### MKUTANO KUHUSU USALAMA WA MTOTO

Mkutano wa usalama wa mtoto

**27.-**(1) Pale ambapo kufuatia uchunguzi wa kijamii, afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri atahitimisha kwa mujibu wa kanuni ya 26(4)(c) kwamba mtoto anadhurika au yupo kwenye hatari ya kudhurika lakini haihitaji kuchukuliwa hatua za haraka ili kumlinda mtoto, afisa ustawi wa jamii anayepokea mashauri atakabidhi suala hilo kwa afisa ustawi wa jamii aliyeteuliwa na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kulishughulikia shauri la mtoto huyo.

(2) Mtumishi wa ustawi wa jamii aliyeteuliwa atapaswa kuitisha mkutano kuhusu usalama wa mtoto ndani ya siku kumi (10) baada ya kukamilisha.

(3) Madhumuni ya mkutano yatakuwa ni kuwawezesha wataalam waliojihusisha na mtoto na familia

yake kupitia taarifa zote muhimu na kupanga namna ya kumlinda mtoto na kuendeleza ustawi wa mtoto huyo.

(4) Afisa ustawi wa jamii atamwalika mtu yeyote mwenye mchango muhimu, ikijumuisha -

(a) wazazi wa mtoto;
(b) ndugu na mlezi yeyote;
(c) afisa ustawi wa jamii aliyemfanyia mtoto au familia uchunguzi wa jamii;
(d) ndugu au familia ya kambo au mtu mwingine aliyemlea mtoto;
(e) wataalam waliohusika na mtoto, wakijumuisha daktari yeyote, nesi, mwalimu, mlezi wa mtoto au mwanasaikolojia;
(f) polisi;
(g) mtu mwingine yeyote ambaye afisa ustawi wa jamii ataona ni wa muhimu.

(5) Mkutano kuhusu usalama wa mtoto -

(a) utaziweka pamoja taarifa kuhusu afya, maendeleo na ustawi wa mtoto na uwezo wa wazazi, mlezi au msimamizi kuhakikisha usalama wa mtoto na kukuza afya na maendeleo ya mtoto;
(b) utafikia maamuzi kuhusu uwezekano wa mtoto kudhurika kwa siku za baadae; na
(c) utapendekeza hatua gani zinazopaswa kuchukuliwa baadae ili kumlinda mtoto, namna gani hatua hizo zitakavyochukuliwa na matokeo yanayotarajiwa.

(6) Kamishna anaweza kutoa miongozo ya kuusaidia mkutano kuhusu ustawi wa mtoto kwa utaratibu, mchakato, maamuzi.

Ushiriki wa mtoto na ndugu katika mkutano wa usalama wa mtoto

**28.-**(1) Wazazi au mlezi, na mtoto mwenye umri na ukomavu wa kutosha watajulishwa kuhusu dhumuni la mkutano, washiriki wa mkutano na namna utakavyofanyika.

(2) Mzazi au mlezi anaweza kumwalika wakili, rafiki au msaidizi ili kuwasaidia katika mkutano.

(3) Mzazi au mlezi -

(a) anayetuhumiwa kumdhalilisha mtoto;
(b) aliyeshtakiwa kwa kutenda jinai dhidi ya mtoto; au
(c) ambaye uwepo wake kwenye mkutano unaweza kupelekea vurugu au udhalilishaji wa mtoto au mtu mwingine,

mwenyekiti hatamjumuisha kwenye mkutano kuhusu usalama wa mtoto.

(4) Endapo mzazi, mlezi au msimamizi hajajumuishwa, hawezi au hataki kushiriki mkutano mzazi huyo au mlezi ataruhusiwa kutoa maelezo yake kwa maandishi na yatasomwa na wajumbe wa mkutano au anaweza kuwasilisha ushahidi wa mdomo kupitia kwa wakili, rafiki, msaidizi au mjumbe wa mkutano isipokuwa mtoto.

(5) Mtoto atapewa fursa ya kuhudhuria kwenye mkutano kuhusu ustawi wa mtoto na atapewa haki ya kuwa na wakili, rafiki au msaidizi endapo atahitaji.

(6) Pale ambapo mtoto atapenda kuhudhuria kwenye mkutano kuhusu ustawi wa mtoto lakini hana uwezo wa kumpata wakili au msaidizi, afisa ustawi wa jamii atatumia uwezo wake kumpata mtu wa kumsaidia mtoto.

(7) Pale ambapo afisa ustawi wa jamii anayehusika na shauri la mtoto atakapoona kuwa endapo atahudhuria haitakuwa ni kwa maslahi ya mtoto, afisa ustawi wa jamii atatathmini matarajio na hisia za mtoto na kuziwasilisha kwenye mkutano.

Taarifa kwenye mkutano wa usalama wa mtoto

**29.-**(1) Afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa atahakikisha kwamba mkutano unakuwa na taarifa zifuatazo-

(a) mlolongo wa matukio ikijumuisha mawasiliano kati ya mtoto na familia na polisi, wataalam wa afya na elimu na mamlaka za serikali za mitaa na asasi za kiraia;

(b) taarifa kuhusu afya na maendeleo ya mtoto;

(c) taarifa kuhusu uwezo wa wazazi, mlezi, msimamizi na ndugu wengine wanaolinda na kuendeleza afya na maendeleo ya mtoto;

(d) maoni yaliyotolewa kuhusu matarajio ya mtoto; na

(e) mchanganuo wa hatari za baadaye kwa usalama, afya na maendeleo ya mtoto.

(2) Afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa atawataka wataalam walioalikwa kuhudhuria mkutano na ambao hawawezi kuhudhuria, kuwasilisha taarifa zao kwa maandishi zinazohitajika chini ya kanuni hizi angalao siku mbili kabla kikao kuhusu usalama wa mtoto hakijaanza.

Mwenyekiti wa mkutano wa usalama wa mtoto

**30.-**(1) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2), atamteua mtu yeyote kuwa Mwenyekiti wa mkutano wa usalama wa mtoto.

(2) Mwenyekiti wa mkutano wa usalama wa mtoto -

(a) kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), hatakuwa mwajiriwa wa idara ya ustawi wa jamii au mjumbe wa kuteuliwa kutoka mamlaka ya serikali ya mtaa.

(b) anaweza kuwa mjumbe wa Kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, au mtu mwingine yeyote ambaye mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ataona kuwa ana uzoefu na uelewa;

(c) atakuwa ni mtu -

(i) mwenye uelewa kuhusu ustawi na maendeleo ya mtoto;

(ii) mwenye uzoefu wa kufanya kazi na watoto; na

(iii) mwenye uelewa kuhusu majukumu ya mwenyekiti.

(3) Kamishna anaweza kuelekeza mafunzo yafanyike kabla mtu yeyote hajawa mwenyekiti wa mkutano kuhusu usalama wa mtoto na utahakikisha kwamba watu hao wanaweza kupata vifaa vya mafunzo**.**

Wajibu wa mwenyekiti wa mkutano wa usalama wa mtoto

**31.** Jukumu la mwenyekiti litakuwa –

(a) kuhakikisha kwamba wajumbe wote wanaohudhuria mkutano wanaelewa lengo la mkutano na nini kitaendelea kwenye mkutano;

(b) kuandaa agenda;

(c) kuwakumbusha watu wote kuwa kikao ni cha siri;

(d) kuwawezesha wote waliohudhuria kuchangia kwa ukamilifu katika mijadala na katika maamuzi;

(e) kuhakikisha kwamba mkutano kuhusu usalama wa mtoto inazingatia taarifa zote ilizo nazo na maoni ya washiriki wote na matarajio ya mtoto;

(f) kuakikisha kwamba miongozo yoyote iliyotolewa na kamishna kwa mujibu wa kanuni ya 27(7) kuhusu utaratibu na mchakato wa mkutano kuhusu usalama wa mtoto unafuatwa.

Majadiliano ya kitaalam kwenye mkutano wa usalama wa mtoto

**32.-**(1) Kabla ya kuanza kwa mkutano kuhusu usalama wa mtoto, mwenyekiti atawakumbusha watu wote waliohudhuria kwamba kutakuwa na majadiliano ya wataalam kuhusu ushahidi uliopo, na wakati huo mwenyekiti atamkata mtoto, wazazi, mlezi au msimammizi na mtu mwingine anayewasaidia kutohudhuria, mkutano wa usalama wa mtoto.

(2) Mwenyekiti anaweza kumtaka mtoto asihudhurie kwenye mkutano wa usalama wa mtoto pale atakapoona kwamba si kwa maslahi ya mtoto kusikiliza taarifa zinazowasilishwa au kujadiliwa na atamfafanulia mtoto ni kwanini ameambiwa asihudhurie.

Muhtasari wa mkutano wa usalama wa mtoto

**33**.-(1) Mwenyekiti atahakikisha katibu amehudhuria ili arekodi muhtasari wa kikao.

(2) Pale ambapo idhini itakapopokelewa na mkuu wa idara ya ustawi wa jamii chini ya kanuni ya 35(9), muhtasari wa mkutano kuhusu usalama wa mtoto -

(a) utasambazwa kwa wataalam wote waliohudhuria;
(b) utasainiwa na mwenyekiti wa mkutano kuhusu usalama wa mtoto;
(c) utajumuisha mapendekezo yoyote yaliyotolewa;
(d) utawasilishwa kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii; na
(e) utawekwa kwenye faili la mtoto.

(3) Mzazi, mlezi au msimamizi aidha amehudhuria au hajahudhuria mkutano wa usalama, baada ya kuomba atastahili kupewa nakala ya maandishi yenye mapendekezo, mpango wowote wa usalama wa mtoto na nakala ya muhtasari, isipokuwa hatapewa nakala inayohusiana na majadiliano ya wataalam.

(4) Pale ambapo afisa ustawi wa jamii aliyeteuliwa endapo mtoto ataomba au akiamini kuwa ni kwa maslahi ya mtoto, atapatiwa nakala ya mapendekezo na mpango wa usalama wa mtoto.

(5) Mtoto au mwakilishi wake anaweza kuomba nakala ya muhtasari inayohusiana na majadiliano ya wataalam.

(6) Mtu yeyote anayehudhuria kwenye mkutano anaweza akafanya mawasilisho kwa mweyekiti wa mkutano wa usalama wa mtoto kuhusu usahihi wa muhtasari na endapo mwenyekiti hatarekebisha muhtasari, mawasilisho hayo yatawekwa kwenye faili la mtoto na nakala itatumwa kwa

mkuu wa idara ya ustawi wa jamii.

Nyaraka kwenye mkutano wa usalama wa mtoto

**34.-**(1) Nyaraka zinazohusiana na mkutano kuhusu usalama wa mtoto hazitachukuliwa baada ya kumalizika kwa mkutano wa usalama wa mtoto au hazitaondolewa kwenye chumba cha mkutano wa usalama wa mtoto isipokuwa na wataalam wanaofanya kazi za mtoto husika.

(2) Nyaraka zote na muhtasari wa mkutano kuhusu usalama wa mtoto zitakuwa ni siri na hazitatolewa kwa mtu yeyote isipokuwa wale waliohudhuria mkutano kuhusu usalama wa mtoto bila ridhaa ya mkuu wa idara ya ustawi wa jamii au kwa amri ya mahakama.

Maamuzi ya mkutano wa usalama wa mtoto

**35.-**(1) Baada ya kuhitimisha mkutano wa usalama wa mtoto, wajumbe ambao ni wataalam, pamoja na mwenyekiti wataamua endapo mtoto bado yupo kwenye hatari ya kudhurika.

(2) Mtoto atachukuliwa kwamba yupo kwenye hatari ya kudhurika endapo ushahidi uliowasilishwa kwenye mkutano wa usalama wa mtoto unaonyesha hivyo kwa uwiano unaowezekana.

(3) Endapo mkutano wa usalama wa mtoto utaona kwamba hakuna ushahidi au ushahidi uliopo haukidhi masharti ya kanuni ndogo ya (2), unaweza -

(a) kupendekeza hatua nyingine isichukuliwe; au

(b) kupendekeza mtoto apelekwe kwenye kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ili kupatiwa huduma.

(4) Kushindwa kwa mzazi, mlezi au mwangalizi kutii wito unaotolewa na Kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi au mamlaka yoyote haitakuwa ni sababu ya kuanza kusikiliza shauri la mtoto upya.

(5) Endapo mkutano wa usalama wa mtoto utahitimisha kwamba mtoto anaguswa na masharti ya kanuni ndogo ya (2), na endapo afya na maendeleo ya mtoto yanaweza kulindwa na mpango wa usalama wa mtoto, mkutano utaandaa muhtasari wa mpango wa usalama wa mtoto kwa mujibu wa kanuni ya 36.

(6) Kukataa kwa mzazi, mlezi au mwangalizi kuridhia mpango wa usalama wa mtoto kutapelekea kutumika njia nyingine chini ya kanuni ndogo ya (8) ili kulinda usalama wa

mtoto.

(7) Endapo mkutano kuhusu usalama wa mtoto utahitimisha kwamba mtoto anaguswa na masharti ya kanuni ndogo ya (2) na kwamba mpango wa usalama wa mtoto hautoshelezi kumlinda mtoto dhidi ya madhara na kumkinga mtoto dhidi ya madhara ya kiafya na kimaendeleo, shauri hilo litarejeshwa kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kwa ajili ya kuchukua hatua za haraka.

(8) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, baada ya kuridhia muhtasari na mapendekezo aliyoyapokea kutoka kwenye mkutano kuhusu usalama wa mtoto, atawasilisha muhtasari huo na mapendekezo kwa mujibu wa kanuni ya 33(2).

Mpango wa usalama wa mtoto

**36.-**(1) Lengo la mpango wa usalama wa mtoto litakuwa -

(a) kumlinda mtoto asidhurike; na

(b) kuboresha afya na maendeleo ya mtoto wakati mtoto yupo nyumbani na mzazi, mlezi au msimamizi.

(2) Pale ambapo itakapokubalika kwamba mtoto atunzwe na ndugu wa familia, mtoto ataendelea kusimamiwa na mpango wa usalama wa mtoto.

(3) Muhtasari wa mpango wa usalama wa mtoto utaandaliwa na mkutano kuhusu usalama wa mtoto kwa kuzingatia matokeo ya ripoti ya uchunguzi wa kijamii na -

(a) utaainisha hatari inayomkumba mtoto na itafafanua namna ambayo mtoto anaweza kulindwa;

(b) utaainisha malengo ya muda mfupi na ya muda mrefu yanayohusiana na kupunguza hatari ya mtoto kudhurika na kuboresha usalama, afya na ustawi wa mtoto;

(c) utafafanua hatua za kuchukua na nani atakayewajibika na utekelezaji wa hatua hizo;

(d) utapanga tarehe ambazo hatua zilizoainishwa kwenye mpango wa usalama wa mtoto zitakamilika;

(e) utazingatia matarajio na hisia za mtoto na maoni ya wazazi, mlezi au msimamizi endapo ni kwa maslahi ya mtoto.

(4) Mwenyekiti wa mkutano wa usalama wa mtoto

atawasilisha mapendekezo ya kikao na muhtasari wa mpango wa usalama wa mtoto kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ambaye, katika kipindi kisichozidi siku saba (7) toka yalipopokelewa, mapendekezo na muhtasari kutoka kwa mwenyekiti kwa kushauriana na na afisa ustawi wa jamii anayehusika na mtoto huyo, atakamilisha mpango wa usalama wa mtoto ndani ya siku 7.

(5) Pamoja na taarifa zilizotajwa kwenye kanuni ndogo ya (3), mpango wa usalama wa mtoto -

(a) utaainisha kwa ufasaha majukumu na wajibu wa wataalam na ndugu wa mtoto yakijumuisha aina na vipindi vya watalam kuwasiliana na mtoto;

(b) utapanga tarehe au sehemu ambazo maendeleo yatafanyiwa mapitio na namna ambayo maendeleo hayo yataamuliwa.

(6) Mpango wa usalama wa mtoto utakuwa kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili (12).

(7) Afisa ustawi wa jamii atawapatia wazazi, mlezi au msimamizi wa mtoto nakala ya mpango wa usalama wa mtoto.

(8) Nakala ya mwisho ya mpango wa usalama wa mtoto itatumwa kwa wataalam wote au watu wote wanaowahudumia watoto endapo wamehudhuria au hawajahudhuria mkutano kuhusu usalama wa mtoto.

(9) Pale ambapo mtoto ana umri wa ukomavu wa kutosha, afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa atamfafanulia mtoto kuhusu mpango wa usalama wa mtoto na atamtaka mtoto akubaliane nao, na makubaliano hayo yatawekwa kwa maandishi.

(10) Pale ambapo mzazi, mlezi, msimamizi au mtoto hatakubaliana na masharti yaliyoko kwenye mpango wa usalama wa mtoto, suala hilo litapelekwa kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii.

(11) Jina la mtoto yeyote anayehusika na mpango wa usalama wa mtoto, litaandikwa kwenye rejesta ya watoto watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi inayohifadhiwa na Idara ya Ustawi wa Jamii.

(12) Jina la mtoto ambaye hahusiki tena na mpango wa usalama wa mtoto litaendelea kubaki kwenye rejesta mpaka atakapotimiza umri wa miaka 18.

Mapitio ya mpango wa usalama wa mtoto

**37.-**(1) Mpango wa usalama wa mtoto utaainisha tarehe za kuufanyia mapitio mpango huo.

(2) Mapitio ya kwanza yatafanyika kabla ya siku ishirini na nane (28) tangu mpango ulipoanza.

(3) Mapitio mengine yatafanyika si zaidi ya miezi mitatu (3) baada ya mapitio ya mwisho endapo mpango wa usalama wa mtoto unaendelea.

(4) Mkutano wa mapitio, kadri itakavyowezekana utaendeshwa na mtu aliyeendesha mkutano wa awali wa usalama wa mtoto.

(5) Watu walioalikwa kwenye mkutano wa mapitio watakuwa ni wale waliohudhuria mkutano kuhusu usalama wa mtoto na mtu mwingine yeyote ambaye mwenyekiti ataona anaweza kukisaidia kikao.

(6) Mwenyekiti atakuwa na mamlaka ya kutomjumuisha mzazi yeyote, mlezi au msimamizi aliyetajwa katika kanuni ya 27(3).

(7) Mkutano wa kufanya mapitio -

(a) utathmini endapo mpango wa usalama wa mtoto bado unalinda maslahi ya mtoto;

(b) utahakikisha kwamba mpango wa usalama wa mtoto umefuatwa na utapendekeza endapo mpango wa usalama wa mtoto uendelee kama ulivyo au ubadilishwe ili kukidhi mahitaji ya mtoto.

(8) Mtoto mwenye umri na ukomavu wa kutosha ataalikwa ili kuzungumza kwenye mkutano wa mapitio na atatoa maoni yake kuhusu utekelezaji wa mpango wa usalama wa mtoto aidha kwa maneno au kwa maandishi na endapo atapendelea, atasaidiwa na afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa au rafiki au mtu anayemuunga mkono atakayemchagua.

(9) Mwenyekiti atahakikisha kwamba katibu anahudhuria ili arekodi muhtasari wa kikao.

(10) Utaratibu wa mkutano wa awali kuhusu usalama wa mtoto chini ya kanuni ya 32 na 33 utatumika kwa kadri itakavyowezekana katika mkutano wa kufanya mapitio.

(11) Kufuatia mkutano wa kufanya mapitio, mwenyekiti baada ya kuzingatia maoni ya wataalam waliohudhuria mkutano wa kufanya mapitio atatoa mapendekezo kwa mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii kwamba -

(a) mpango kuhusu usalama wa mtoto uendelee kama

ulivyoandaliwa tangu awali;

(b) mpango kuhusu usalama wa mtoto urekebishwe;

(c) mpango kuhusu usalama wa mtoto hauna ulazima ili kumlinda mtoto;

(d) ili kumlinda mtoto hatua zaidi inahitajika.

(12) Pale ambapo mapendekezo ni ya kubadilisha mpango kuhusu usalama wa mtoto, mwenyekiti wa mkutano kuhusu usalama wa mtoto atamtaarifu mkuu wa idara ya ustawi wa jamii na kumpatia mapendekezo yoyote ya mabadiliko yanayopaswa kufanywa kwenye mpango kuhusu usalama wa mtoto na sababu ya mabadiliko hayo.

(13) Mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atatathmini mapendekezo kwa pamoja na afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa na kuamua endapo kuyakubali au kuyakataa mapendekezo kutakuwa ni kwa maslahi ya mtoto.

(14) Pale ambapo uamuzi ni wa kuyakataa mapendekezo, mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii anaweza -

(a) kuendelea na mpango uliopo;

(b) kuurekebisha mpango ili kukidhi mahitaji ya mtoto;

(c) kuurejesha mpango kwenye mkutano wa usalama wa mtoto na kutoa maelekezo kuhusu mambo ya kuzingatiwa.

(15) Pale ambapo ushauri umetolewa kwamba mpango wa usalama wa mtoto hauhitajiki tena, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atatathmini mapendekezo hayo na kuamua endapo -

(a) kuyakubali mapendekezo; au

(b) kuyakataa mapendekezo.

(16) Pale ambapo kuna pendekezo la kusitisha mpango wa uangalizi wa mtoto linakataliwa, mpango huo utaendelea kuwa na nguvu, isipokuwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii anaweza kufanya marekebisho kwenye mpango huo kwa kadri ambavyo ataona inafaa.

(17) Iwapo mwenyekiti wa mkutano wa uangalizi wa mtoto anasababu za kuamini, katika muda wowote, ikijumuisha mwishoni mwa kipindi cha miezi kumi na miwili cha mpango wa uangalizi wa mtoto, bila kujali mpango wa uangalizi wa mtoto, kuwa mtoto anapata mateso au yuko hatarini kupata mateso, atalirudisha suala hilo kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ndani ya saa sabini na mbili.

(18) Mwenyekiti, iwapo atamua kulirudisha suala kwa mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, atawataarifu wahusika

wote ili wafanye mkutano wa mapitio.

(19) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, baada ya kupokea maombi ya rufaa yaliyo fanywa chini ya kanuni ndogo ya (18), mara moja ataweka maandalizi kwa ajili ya uchunguzi wa ziada wa kijamii kufanyika na kukamilika ndani ya siku saba, na kwa kushirikiana na afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa, wataamua, iwapo itaonekana kuwa ni muhimu, na si zaidi ya masaa sabini na mbili, baada ya kupokelewa kwa taarifa ya uchunguzi ya kijamii, hatua zozote za ziada zitakazo hitajika kuchukuliwa ili kumlinda mtoto dhidi ya athari na kulinda afya na maendeleo yake.

(20) Afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa atawataarifu wazazi kuhusu mabadiliko yoyote yaliyofanyika kwenye mpango wa uangalizi wa mtoto.

## SEHEMU YA TISA
### WATOTO WANAOHITAJI MSAADA NA MALAZI

Wajibu kwa watoto waliopotea, waliotelekezwa, wanaohitaji hifadhi au wasio na uangalizi wa wazazi

**38.-**(1) Mtoto anayeletwa kama, au anayetambuliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama mtoto aliyepotea, aliyetelekezwa, anayetafuta hifadhi au asiye na uangalizi wa wazazi, kwa sababu yoyote ile, atachukuliwa kuwa ni mtoto anayehitaji matunzo na uangalizi kwa maana iliyotolewa na kifungu cha 16 na 144 cha Sheria na Kanuni ya 4.

(2) Mamlaka ya Serikali za Mitaa inayohusika kwa ajili ya mtoto huyo itakuwa ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya eneo ambalo mtoto huyo kikawaida ana makazi.

(3) Pale ambapo mtoto hana sehemu maalum ya makazi, mamlaka ya serikali za mitaa ambayo ndani ya eneo lake mtoto huyo anaonekana kuwa hana uangalizi wa wazazi, amepotea, ametelekezwa au anatafuta hifadhi, kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), itachukua wajibu kuhusiana na mtoto huyo, isipokuwa kwamba masharti ya kanuni hii ndogo hayatakuwa muhimu pale ambapo mamlaka nyingine ya serikali za mtaa tayari imechukua jukumu kuhusiana na mtoto huyo, ambapo katika hali hiyo, mamlaka hiyo itaendelea kutekeleza jukumu hilo kwa ajili ya mtoto huyo.

(4) Wakati uchunguzi wa awali na uchunguzi wa kijamii unaendelea, idara ya ustawi wa jamii atampatia mtoto msaada na malazi chini ya kifungu cha 94(5) cha Sheria, ndani ya wilaya yoyote au wilaya ya mamlaka nyingine ya serikali za

mitaa.

(5) Kabla ya kutoa msaada wa malazi, Idara ya Ustawi wa Jamii, kwa kadri itakvyo wezekana, na kwa kuzingatia ustawi wa mtoto, ita-

(a) hakikisha kuwa matakwa ya mtoto na hisia zake kuhusiana na kutolewa kwa msaada wa malazi; na
(b) zingatia, kwa mujibu wa umri wa mtoto na hali yake ya kupevuka, matakwa na hisia zake kwa kadri ambavyo vitakuwa vimebainishwa.

(6) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii atamtendea mtoto yeyote ambaye anapewa msaada wa makazi chini ya kanuni hii kama mtoto ambaye kwake wamechukua majukumu na haki za mzazi hadi hapo mzazi wake atakapo patikana.

(7) Iwapo-

(a) mtoto ambaye anapewa malazi na msaada chini ya kanuni hii anapinga kurudishwa chini ya uangalizi wa mzazi au mlezi au mwangalizi;
(b) afisa ustawi wa jamii anaamini kuwa kuondolewa kwa mtoto kutoka katika malazi kunaweza kumsababishia mtoto huyo matatizo,

afisa huyo wa ustawi wa jamii atawasilisha suala la mtoto huyo kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii, ambaye atatoa uamuzi ndani ya saa sabini na mbili, hatua za ziada, ikijumuisha kumuweka mtoto kwenye mahali usalama kwa mujibu wa kanuni ya 22, iwapo itaonekana ni muhimu kwa ajili ya usalama wa mtoto huyo.

(9) Pale ambapo haiwezekani kumkutanisha mtoto, ambaye katika masharti ya kifungu cha 94(5) cha Sheria, anatambulika kuwa ni mtoto aliyepotea, aliyetelekezwa au anaye hitaji hifadhi ya wazazi wake, mlezi au mwangalizi au iwapo wazazi wa mtoto huyo wamefariki, hawawezi kupatikana au hawana uwezo au anaangukia chini ya masharti ya kanuni ya 39, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii, baada ya kufanyika kwa uchunguzi awali na uchunguzi wa kijamii kufanyika kwa mujibu wa kanuni ya 14 na 26, atatoa uamuzi kuhusu hatua za ziada, iwapo zipo, ambazo ni muhimu kwa ajili ya kulinda ustawi wa mtoto, ikijumuisha-

(a) kuwekwa chini ya uangalizi wa ndugu;
(b) kuwekwa chini ya uangalizi wa kale wa hiari;
(c) kufanya maombi ya amri uangalizi au usimamizi kuhusiana na mtoto.

Rufaa ya mtoto anaye vunja sheria

**39.-**(1) Pale ambapo mtoto-
(a) ametiwa mbaroni au anawekwa kizuizini na polisi;
(b) ameachiliwa kutoka katika mahabusu ya watoto au jela kutokana na kufutwa kwa mashitaka dhidi yake;
(c) ameachiliwa kwa kosa na mahakama;
(d) ametiwa hatiani ka kosa na anapewa kifungo cha nje,

na mtoto, kwa sababu yoyote ile, anakuwa hana uangalizi wa wazazi, mzazi hawezi kupatikana, wazazi hawako tayari kumtunza mtoto huyo, itachukuliwa kuwa kuwa mtoto yuko hatarini kupata madhara na rufaa ya uangalizi itatolewa na polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka, Mahakama au Shule ya Maadilisho kwa mujibu wa kanuni ya 12.

(2) Rufaa ya uangalizi wa mtoto uliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) itapelekwa kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ambamo kikawaida mtoto huyo ana makazi.

(3) Iwapo mtoto hana mahali maalum pa kuishi, mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii wa wilaya-
(i) ambayo kituo cha polisi kipo, iwapo ni mtoto anayeangukia chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (1)(a); au
(ii) katika wilaya ambayo mtoto huyo alikamatwa au wilaya ambayo mahakama ipo, iwapo ni mtoto anayeangukia chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (1)(b), (c) au (d).

(4) Mtoto anayeangukia chini ya kanuni ndogo ya (1) anaweza kupewa msaada na malazi kwa mujibu wa kifungu cha 94(5) cha Sheria, katika wilaya nyingine iwapo-
(a) malazi yanayokidhi mahitaji yanapatikana;
(b) itamuwezesha mtoto kushiriki katika programu ya mchepuko au marekebisho.

(5) Kununi za 38(3)-(9) zitatumika kwa watoto wanaopewa msaada au malazi chini ya kanuni ndogo ya (3).

Uangalizi wa mtoto anaye vunja sheria

**40.-**(1) Pale ambapo mtoto ameshitakiwa kwa kutenda kosa la jinai na dhamana haijatolewa kutokana na sababu kuwa mtoto hana mtu wa kumtunza au hana malazi au hana mtu wa kumwekea dhamana mahakama inaweza kuamuru kuwa mtoto huyo awekwe chini ya uangalizi wa Kamishna kwa mujibu wa

kifungu cha 104(2) cha Sheria na mtoto apewe msaada na malazi chini ya kifungu cha 94(5) cha Sheria hadi ambapo shitaka litakapofutwa au uamuzi umefikiwa.

(2) Pale ambapo amri iliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) inatolewa na mahakama, Kamishna atakasimisha uangalizi wa mtoto kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii wa wilaya ambayo mtoto kikawaida na makazi au iwapo mtoto hana mahali pa kudumu pa kuishi, kwenye wilaya ambayo mtoto alikamatwa au idara nyingine ya ustawi wa jamii, kwa kadri ambavyo Kamishna ataona inafaa, isipokuwa kwamba, iwapo mamlaka nyingine ya serikali za mitaa imechukua jukumu kuhusiana na mtoto huyo, iwapo itakuwa na uwezo, itaendelea kumtunza mtoto huyo kwa niaba ya Kamishna, kwa madhumuni yaliyo ainishwa kwenye kanuni hii.

(3) Mtoto hataondolewa kutoka kwenye uangalizi wa idara ya ustawi wa jamii inayohusika au kutoka katika malazi yanayotolewa kwake bila ya amri ya mahakama.

Wajibu wa mtoto aliyehamishwa

**41**.-(1) Pale ambapo mtoto, ambaye ni wajibu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, anapewa msaada na malazi chini ya kanuni za 38 hadi 40 katika wilaya ya idara nyingine ya ustawi wa jamii, idara ya ustawi wa jamii ambayo mtoto amewekwa chini yake itawajibika kwa ajili ya mtoto huyo.

(2) Kamishna wa ustawi wa jamii atakuwa na mamlaka ya kuandaa Kanuni na Miongozo kuhusu kuhamishwa kwa fedha kwa ajili ya watoto wanaolelewa nje ya wilaya ambayo kikawaida mtoto huyo ana makazi.

Kuwekwa chini ya uangalizi wa kujitolea

**42.**-(1) Pale ambapo-

(a) mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, kwa kuzingatia taarifa ya uchunguzi ya kijamii, ana sababu za msingi za kuamini kuwa mtoto yuko hatarini kupata madhara iwapo mtoto huyo hatawekwa chini ya uangalizi; au

(b) mkutano wa uangalizi wa mtoto umelirejesha shauri la mtoto kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 37(15);

mkuu wa idara ya ustawi wa jamii kwa kuzingatia kuwa-

(a) idhini ya wazazi ya mtoto kuwekwa chini ya uangalizi inapatikana; na

(b) kwa mtoto ambaye anaangukia chini ya masharti ya kanuni ya 38-
   (i) haiwezekani kumuunganisha mtoto huyo na wazazi wake; au
   (ii) mzazi hawezi, kwa sababu yoyote ile, kumlea mtoto huyo; na
   (iii) kwa kumuweka mtoto huyo chini ya uangalizi wa ndugu, itakuwa ni vigumu kuhakikisha ustawi wa mtoto huyo,

atamuweka mtoto huyo chini ya uangalizi wa hiari wa mamlaka ya serikali za mitaa.

(2) Mpango wa uangalizi utaandaliwa kwa ajili ya mtoto na afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa kabla mtoto huyo hajawekwa chini ya uangalizi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, isipokuwa kwamba, iwapo mtoto anawekwa chini ya uangalizi wa hiari kwa mzingira ya dharura, mpango wa uangalizi wake utaandaliwa ndani ya siku ishirini na moja.

(3) Katika kuandaa mpango wa uangalizi wa mtoto, idara ya ustawi wa jamii itazingatia vigezo vilivyo ainishwa kwenye Kanuni ya 48, na muongozo wowote muhimu utakaotolewa na Kamishna.

(4) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii atazipitia upya taarifa za uchunguzi wa awali na uchunguzi wa kijamii na mpango wa uangalizi ulioandaliwa na kujiridhisha kabla ya kukubali kumpokea mtoto chini ya uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa, kwamba-

(a) mtoto huyo yuko ndani ya masharti ya kanuni ndogo ya (1);
(b) ni vigumu kuhakikisha ustawi wa mtoto huyo kwa kuwapa wazazi wake msaada ili waendelee kumlea mtoto huyo;
(c) hakuna ndugu ambao wanaweza kumlea na kuhakikisha ustawi wa mtoto huyo; na
(d) kuna uwezekano wa mtoto huyo kukapata madhara iwapo atawekwa chini ya uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa.

(5) Pale ambapo mtoto anatakiwa kuwekwa chini ya uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa chini ya kanuni ndogo ya (1), afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa atakubaliana na mzazi kuhusu mpango wa atamfafanulia mzazi -

(a) kuhusu madhara ya mtoto kuwekwa chini ya uangalizi wa serikali za mitaa;
(b) kwamba notisi ya siku kumi na nne itatakiwa kabla ya kumuondoa mtoto kutoka katika uangalizi wa hiari na kwamba kusudio hilo la kumuondoa litafanyiwa mapitio, isipokuwa kama kuwekwa chini ya uangalizi wa hiari kulikuwa ni kwa masharti ya muda na kwa kipindi fulani kilichokubaliwa;
(c) kwamba mamlaka ya serikali za mitaa zinaweza kuchagua kuiomba mahakama amri ya uangalizi iwapo ina sababu za msingi kuamini kuwa kitendo hicho ni muhimu kuhakikisha ustawi wa mtoto;
(d) kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa itachangia haki na wajibu wa mtoto na wazazi wa mtoto huyo na itaamua sehemu ambayo na nani atakayeishi na mtoto huyo;
(e) utaratibu kuhusiana na namna ya kumuonana baina ya mtoto na wazazi wake na watu wengine muhumu katika maisha ya mtoto huyo; na
(f) kwamba mzazi ataalikwa wakati wa kufanya mapitio ya mpango wa uangalizi.

(6) Idhini ya mzazi kuhusu kwa mtoto kuwekwa chini ya uangalizi chini ya kanuni ndogo ya (1)(a) itanalikiwa rasmi kwa maandishi na mkuu wa idara ustawi wa jamii.

(7) Mtoto hatawekwa chini ya uangalizi iwapo kuna uwezekano wa yeye kupata madhara unatokana kipekee au kwa kiasi kikubwa na umasikini, isipokuwa anaweza kupelekwa kwenye Kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ili kupata huduma.

(8) Pale ambapo mtoto anapokelekwa kwenye uangalizi kwa idhini ya wazazi na makubaliano hayakuweza kufikiwa na wazazi kuhusiana na mpango wa uangalizi, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atazingatia iwapo ni kwa manufaa ya mtoto kwa mamlaka ya serikali za mitaa kufanya maombi ya amri ya uangalizi.

(9) Mtoto yeyote aliyepokelewa kwa ajili ya uangalizi chini ya kanuni hii atakuwa na hadhi kisheria sawa na mtoto ambaye yuko chini ya amri ya uangalizi, na mamlaka ya serikali za mitaa itakuwa na wajibu ule ule sawa za ule wa mtoto aliye chini amri ya uangalizi au mtoto ambaye anapewa

msaada na malazi chini ya kanuni ya 94(5) ya Sheria.

Kusitishwa kwa huduma ya uangalizi wa hiyari

**43**.-(1) Mzazi anayetaka kusitisha malezi ya mtoto wake chini ya uangalizi kwa hiari, atampatia mkuu wa idara ya ustawi wa jamii notisi ya siku kumi na nne, ama kwa maneno au kwa maandishi ya kusudio lake la kumtoa mtoto kutoka kwenye uangalizi wa hiari na maelezo ya namna ambavyo mazingira yamebadilika na mpangilio wa namna ya kumtumza mtoto huyo, ikijumuisha sehemu ambayo mtoto ataishi, ataishi na nani na mpangilio wa elimu au huduma muhimu za kiafya.

(2) Notisi iliyotlewa chini ya kanuni ndogo ya (1) itatosha kumuwezesha mtoto kuondolewa chini ya uangalizi wa hiari na kumrudisha kwa wazazi wake, isipokuwa kwamba, iwapo mkuu wa idara ya ustawi wa jamii anasababu za msingi kuamini kuwa mtoto huyo anaweza kupata madhara kwa kuondolewa chini ya uangaizi hiari na mzazi, afisa ustawi wa jamii anaweza kumuweka mtoto huyo kwenye mahali salama kwa mujibu wa kanuni ndogo ya 22(3), ili kumzuia mzazi kumtoa mtoto kutoka kwenye sehemu ya uangalizi.

(3) Pale ambapo mtoto amewekwa kwenye mahali salama taratibu za uangalizi wa mtoto zilizoainishwa kwenye Sehemu za Sita na Nane za Kanuni zitatumika.

## SEHEMU YA KUMI
### MAOMBI YA AMRI YA UANGALIZI AU USIMAMIZI

Maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi

**44.-**(1) Pale ambapo mtoto anapata madhara au anaweza kupata madhara kama ilivyotafsiriwa kwenye kanuni ya 4 na iwapo madhara yanatokana na-

(a) uangalizi unaotolewa au unaoweza kutolewa na mzazi kwa mtoto; au

(b) mtoto kuwa na tabia zisizozuilika; na

(c) mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ameamua kuwa ustawi wa mtoto unaweza kulindwa na amri ya uangalizi au usimamizi pekee,

Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza kufanya maombi kwa ajili ya amri ya uangalizi au usimamizi.

(2) Kabla ya kufanya maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atahakikisha kuwa uwezo na utayari wa ndugu kumlinda na kumhudumia mtoto umeazingatiwa na kukutwa kuwa haufai kumlinda mtoto

dhidi ya madhara na kumlinda dhidi ya upungufu kwenye afya na maendeleo ya mtoto.

Mamlaka ya kuomba amri ya uangalizi au usimamizi

**45**.-(1) Maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi yatafanywa na mamlaka ya serikali za mitaa ya eneo ambamo mtoto kikawaida ana makazi au iwapo mtoto hayuko chini ya uangalizi wa mzazi, mlezi au mwangalizi, Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya eneo ambalo mtoto alipatikana au alipopotelea, kutelekezwa au anatafuta hifadhi isipokuwa kama kuna mamlaka nyingine ya serikali **za** mitaa iliyochukua jukumu la kumwangalia mtoto huyo.

(2) Maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi yatafanywa kwenye mahakama kwa mujibu wa Kanuni za Mahakama ya Watoto.

Kuwataarifu watu kuhusu kusudio la kufanya maombi ya amri uangalizi au usimamizi

**46.**-(1) Kabla maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi hayajafanywa, idara ya ustawi wa jamii ita-

(a) kwa mdomo na kwa maandishi, kwa kutumia lugha na njia za mawasiliano zinazoelekweka kwa urahisi zaidi, itawaarifu wazazi wote-

(i) kuwa mamlaka ya serikali za mitaa inakusudia kufanya maombi kwa ajili ya amri ya uangalizi au usimamizi;

(ii) hali na maoni ya mamlaka ya serikali za mitaa; na

(iii) haki yao ya kuwakilishwa na njia zilizopo za upatikanaji wa ushauri wa kisheria.

(b) mtaarifu mtoto aliye na umri wa kuelewa na aliye na umri wa utu uzima, kusudio lake la kufanya maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi, isipokuwa kama kufanya hivyo ni kwa manufaa ya mtoto.

(2) Pale ambapo mtoto ame-

(a) potea, telekezwa au anatafuta hifadhi; na

(b) mama, baba yake, mlezi au mwangalizi wake hawajulikani au hawawezi kupatikana, baada ya uchunguzi unaostahili kufanyika;

(c) mama , baba yake, mlezi au mwangalizi wake hawana uwezo, idara ya ustawi wa jamii inaweza kufanya maombi na kupata ridhaa ya makahakama

wakati wa hatua za awali za kusikilizwa kwa shauri ili iweze kuendelea pasipo kumtaarifu mzazi

(3) Uchunguzi utachukuliwa kuwa umefanyika kikawaida chini ya kanuni ndogo ya (2)(b) iwapo-

(a) uchunguzi kuhusu mahali wazazi walipo umefanyika katika sehemu ambayo inaaminika kuwa wazazi hao wanaishi;

(b) uchunguzi umefanyika kwa mwajiri wake wa mwisho anayefahamika; na

(c) uchunguzi umefanyika kwa mtu yeyote ambaye kikawaida anaweza kutarajiwa kujua sehemu ambayo mzazi anakaa.

(4) Iwapo, katika hali ambayo mkuu wa idara ya ustawi wa jamii anaamua kufuata uchunguzi halisi au uchunguzi wa kijamii ya kwamba si muhimu kumuondoa mtoto kwenye sehemu ya usalama, isipokuwa kwamba maombi ya dharura kwa ajili ya amri ya uangalizi au usimamizi yanahitajika ili kuhakikisha usalama wa mtoto, Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza kufanya maombi pasipo Idara ya Ustawi wa Jamii kwanza kuwasilisha taarifa zilizo ainishwa kwenye kanuni ndogo ya (1)(a).

(5) Pale ambapo masharti ya kanuni ndogo ya (4) yanatumika, mzazi, mlezi, muangalizi au msimamizi atapewa taarifa zilizoainsihwa kwenye kanuni ndogo ya (3) si zaidi ya tarehe ya kwanza ya kusikilizwa kwa shauri mahakamani.

Nyaraka zitakazo wasilishwa pamoja na maombi ya amri ya uangalizi au usimamizi

**47**.-(1) Pale ambapo maombi yanafanywa kwa ajili ya amri ya uangalizi au usimamizi, Idara ya Ustawi wa Jamii, kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, itawasilisha nyaraka zifuatazo mahakamani-

(a) maelezo ya maandishi-

(i) yanayoelezea maisha ya awali ya familia ya mtoto;

(ii) yanayoelezea athari halisi au inayoweza kumpata mtoto huyo;

(iii) yanayoainisha matakwa na hisia za mtoto;

(b) mpango wa uangalizi au mpango wa usimamizi kwa ajili ya malezi ya baadaye ya mtoto;

(c) taarifa ya uchunguzi wa awali, kama ipo;

(d) taarifa ya uchunguzi wa ustawi wa jamii, kama ipo;

(e) ushahidi kwamba mzazi, mlezi, au muangalizi ametaarifiwa kuhusu kusudio la mamlaka ya serikalia ya mitaa kufanya maombi kwa ajili ya amri ya uangalizi au usimamizi kwa mujibu wa kanuni ya 46; na

Tangazo la Serikali Na. 197 la 2012

(f) iwapo mzazi au mlezi ameridhia kuasiliwa kwa mtoto mbele ya hakimu, kwa mujibu wa kanuni ya 9 ya Kanuni za Uasili wa Watoto, idhini iliyosainiwa.

Maandalizi na yaliyomo katika mpango wa uangalizi

**48**.-(1) Mpango wa uangalizi utaandaliwa kwa mujibu wa muongozo wowote utakaotolewa na Kamishna na utajumuisha-

(a) maandalizi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya mtoto kuhusiana na-
   (i) afya yake, ikijumuisha afya ya kimwili na afya ya akili;
   (ii) elimu na mafunzo;
   (iii) maendeleo ya kihisia na kitabia;
   (iv) utambuzi wake, kwa kuzingatia imani ya kidini asili ya ubini na taarifa kuhusu utamaduni na lugha yake ya asili;
   (v) mahusiano ya kifamilia na kijamii na mawasiliano ambayo mtoto atakuwa nayo na familia yake na namna na mahali ambapo yatafanyika;
   (vi) sehemu ya uangalizi; na
   (vii) ujuzi wa wakijamii na ujuzi wa kuji**tunza** mwenyewe;

(b) mpango wa muda mrefu wa malezi ya mtoto, ikijumuisha kuasiliwa, iwapo itakuwa ni kwa manufaa ya mtoto huyo; na

(c) kiwango cha mawasiliano ambacho mtoto atakuwa nacho na wazazi wake na watu wengine muhimu katika maisha ya mtoto huyo chini ya amri ya mpito au amri kamili ya uangalizi.

(2) Mpango wa uangalizi, kwa kadri itakavyowezekana kawaida kabisa, utakubaliwa na kusainiwa na afisa ustawi wa jamii na-

(a) mzazi, mlezi au muangalizi;

(b) mtoto, iwapo ana umri wa uelewa na ni mtu mzima;

(3) Mpango wa uangalizi utafanyiwa mapitio wakati mwenendo unaendelea na unaweza kufanyiwa marekebisho ili kuonyesha mabadiliko katika mazingira na mahitaji ya mtoto.

(4) Mpango wa uangalizi utachukuliwa kuwa ni wa mwisho, iwapo, pamoja na taarifa iliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya 1(a) na (c), una-

(a) ainisha kwa ukamilifu majukumu na wajibu wa wanataaluma na ndugu, ikijumuisha hali na idadi ya mawasiliano baina ya wanataaluma na mtoto; na

(b) taja tarehe ya mapitio ya mwanzo.

(5) Mpango wa mwisho wa uangalizi utawasilishwa si zaidi ya wiki mbili kabla ya shauri kusikilizwa kwa mara ya mwisho.

Pale ambapo mzazi anakubali kuasiliwa

**49.-**(1) Pale ambapo Mamlaka ya Serikali za Mitaa inakusudia kuwasilisha maombi kwa ajili ya amri ya uangalizi, na mpango wa uangalizi unabainisha kuwa kuasiliwa ndiyo njia bora ya kulinda maslahi ya mtoto, afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa atamuuliza mzazi au mlezi iwapo anaridhia mtoto aasiliwe.

(2) Pale ambapo watu waliotajwa kwenye kanuni ndogo ya (1) wako tayari kukubali idhini hiyo itakuwa kwa maandishi na itasainiwa mbele ya hakimu kwa mujibu wa Kanuni za Uasili wa Watoto.

Tangazo la Serikali Na. 197 la 2012

(3) Mtu ambaye mbele yake idhini imesainiwa atamtaarifu mtu anayetoa idhini hiyo kuhusu-

(a) madhara ya kuasiliwa huko; na

(b) haki ya kutengua idhini ndani ya siku sitini, kwa mujibu wa utaratibu uliyowekwa na kanuni ya 9 ya Kanuni za Uasili wa Watoto.

(4) Pale ambapo mamlaka ya serikali za mitaa imefanya maombi kwa ajili ya amri ya uangalizi na wazazi, mlezi au watu wenye na haki ya uzazi na majukumu yalitolewa chini ya makubaliano au amri ya mahakama, wameridhia uasili huo kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), mahakama itaweka kumbukumbu kuwa mtoto yuko huru kwa ajili ya kuasiliwa na anaweza kupelekwa kwa wazazi wake waliomuasili.

(5) Ridhaa ya wazazi au mlezi kuhusiana na uasili au kumpeleka mtoto kwa wazazi waliomuasili hakitaondoa hitaji

ya watu wanaokusudia kumuasili mtoto kufuata masharti yaliyotolewa kwenye Kanuni za Uasili wa Watoto au kufanya maombi kwa ajili ya kuasili amri ya kuasili kwa mujibu wa Sheria.

(6) Iwapo mahakama imeweka kumbukumbu kuwa mtoto yuko huru kuasiliwa chini ya kanuni ndogo ya (4), maombi ya amri ya kuasili hayatataja jina la wazazi, mlezi au mtu aliye na haki za malezi na wajibu chini ya mkataba au amri ya mahakama kama mhusika katika maombi ya kuasili.

Kuondokana na idhini ya kuasili

**50**.-(1) Pale ambapo Mamlaka ya Serikali za Mitaa inawasilisha maombi kwa ajili ya amri ya uangalizi na mpango wa uangalizi ni wa uasili na-

(a) mzazi au mlezi hawezi kupatikana;

(b) mmoja au wote kati ya wazazi wa mlezi hawajulikani; au

(c) wazazi au mlezi hawana uwezo wa kutoa idhini,

maombi kwa ajili ya kuondokana na idhini ya mzazi yanaweza kuafanywa katika muda huo huo ambapo maombi ya amri ya uangalizi yanafanyika au katika muda wowote wakati wa mwenendo unaendelea.

(2) Pale ambapo mamlaka ya serikali za mitaa inafanya maombi kwa ajili ya amri ya uangalizi kuhusiana na uasili, ambapo katika hali hiyo-

(a) wazazi au walezi hawaridhii uasili huo; au

(b) wazazi au walezi wamemtelekeza, wameshindwa kumlea, hawamtunzi au kwa mfululizo wanamnyanyasa mtoto au wameshindwa kumlinda mtoto dhidi ya kutelekezwa au kunyanyaswa kwa mfululizo na mtu mwingine,

mamlaka ya serikali za mitaa inaweza kufanya maombi kwa ajili ya kuondokana na hitaji la idhini ya mzazi kwa ajili ya kuasili wakati wa kuwaislisha maombi ya amri ya uangalizi au katika muda wowote wakati mwenendo wa shauri kwa kigezo kuwa idhini inazuiliwa pasipo kuwa na sababu ya msingi.

(3) Wakati wa kufanya maombi ya kuondokana na hitaji la idhini, mamlaka ya serikali za mitaa itawasilisha ripoti pamoja na ushahidi unahitajika chini ya kanuni ya 47, utakaoinisha-

(a) sababu na ushahidi uliotumika kuiondoa idhini;

(b) uwezekano wa mtoto kuunganishwa tena na

familia yake ya kuzaliwa ndani ya muda unaoendana na mahitaji ya mtoto;

(c) muda ambao mtoto amehudumiwa akiwa nje ya familia, iwapo kuna mazingira kama hayo;

(d) vipindi vya mawasiliano kati ya mtoto na wazazi, mlezi au mtu mwingine ambaye ana haki ya uzazi na wajibu chini ya mkataba au amri ya mahakama; na

(e) sababu za kwani inadaiwa kuwa idhini inazuiliwa bila sababu za msingi.

(4) Pale ambapo mahakama inaondokana na idhini iliyotolewa chini ya kanuni hii, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii anaweza kuidhinisha mtoto kupelekwa kwa wazazi wake wa kuasili watarajiwa.

Tangazo la Serikali Na. 197 la 2012

(5) Kuondokana na idhini au kuwekwa chini ya malezi ya wazazi wa kuasili hakutaondoa hitaji la wazazi wa kuasili kutekeleza masharti ya Kanuni za Uasili wa Watoto au kuomba amri ya uasili chini ya Sheria.

(6) Pale ambapo idhini imeondolewa chini ya kanuni ya 127 ya Kanuni za Mahakama ya Watoto na mtoto ameasiliwa na amri ya kuasili imetolewa, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atawajulisha wazazi, mlezi au mtu yeyote aliye na haki na wajibu wa malezi chini ya makubaliano au amri ya mahakama kuwa amri ya kuasili imetolewa.

Amri ya usimamizi

**51.** Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza kufanya maombi kwa ajili ya usimamizi kwa ajili ya kuzuia mtoto kupata madhara wakati mtoto huyo yuko kwenye nyumba ya familia chini ya uangalizi wa wazazi, mlezi wake au ndugu yake.

Mpango wa usimamizi

**52.-(**1) Wakati wa kufanya maombi kwa ajili ya amri ya usimamizi, Idara ya Ustawi wa Jamii itawasilisha mpango wa usimamizi wa mtoto, ambao utaainisha namna ambavyo mahitaji ya muda mfupi ya mtoto yatashuguulikiwa, kwa mujibu wa muongozo wowote utakaotolewa na Kamishna.

(2) Mpango wa usimamizi utajumuisha-

(a) sehemu ambayo mtoto ataishi kwa kipindi cha utekelezaji wa amri ya usimamizi;

(b) msaada utakaotolewa na idara ya ustawi wa jamii au vyombo vingine kwa mtoto na familia;

(c) shughuli zozote za kielimu au mafunzo ambazo mtoto au wake wanatarajiwa kuhudhuria;
(d) sehemu zozote maalum ambazo mtoto anatarajiwa kwenda katika vipindi maalum;
(e) mahudhurio kwenye hospitali au mpango wa tiba au wa matibabu;
(f) wajibu wowote ambao wazazi wanatarajiwa kutekeleza; na
(g) masharti mengine kwa kadri ambavyo idara ya ustawi wa jamii itaona ni muhimu kwa ajili ya usalama wa mtoto.

(3) Mpango wa usimamizi hautamtaka mtoto kuishi sehemu nyingine yoyote mbali na familia yake.

Mamlaka ya usimamizi

**53**.-(1) Kwa kuzingatia kanuni ya 39 ya Kanuni za Mahakama ya Watoto, mtoto ambaye anahusika na amri ya uangalizi atawekwa chini ya uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa inayoomba uangalizi, isipokuwa kwamba, iwapo mtoto ataishi katika eneo lingine la mamlaka ya serikali za mitaa, mtoto huyo atawekwa chini ya uangalizi wa mamlaka hiyo ya serikali za mitaa kwa kipindi cha amri hiyo.

(2) Pale ambapo mpango wa usimamizi ni kwamba mtoto aishi kwenye mamlaka ya serikali za mitaa, mbali na mamlaka iliyofanya maombi, mamlaka ya serikali za mitaa ambayo haikufanya maombi itaarifiwa wakati mpango wa usimamizi umewasilishwa mahakamani.

(3) Afisa ustawi wa jamii kutoka katika wilaya ambayo mtoto ataishi kwa kipindi cha amri hiyo, atapangiwa kumsimamia mtoto huyo, isipokuwa kwamba, iwapo idara ya ustawi wa jamii haina uwezo, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii anaweza kumtea mtu anayestahili kusimamia.

(4) Katika kumpangia mtu anayestahili, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atahakikisha kuwa mtu huyo ana uzoefu wa kushughulikia watoto na amepata mafunzo kwa kadri ambavyo imeelekezwa na Kamishna.

(5) Mtu stahili ambaye amepangiwa kumsimamia mtoto atasimamiwa na afisa ustawi wa jamii na atatoa taarifa kwa afisa huyo wa ustawi wa jamii kuhusuiana na maendeleo ya usimamizi mara moja kwa mwezi.

Wajibu wa msimamizi

**54**.-(1) Wakati amri ya usimamizi inaendelea kutumika, itakuwa ni wajibu wa msimamizi-

(a) kumshauri, kumsaidia na kumfanya mtoto anayesimamiwa kuwa karibu yake;

(b) atachukua hatua ambazo kikawaida ni muhimu kwa ajili ya kuandaa mpango wa usimamizi;

(c) iwapo-

(i) mpango haujatekelezwa kikamilifu;

(ii) mzazi au mlezi ambaye mtoto anaishi naye anamnyima msimamizi nafasi ya kumuona mtoto;

(iii) msimamizi anaona kuwa amri ya usimamizi haihitajiki tena,

msimamizi huyo atatoa taarifa kwa mkuu wa idara ya ustawi ambaye ataamua amakuiomba mahakama amri ya kuipitia upya amri ya usimamizi au kutoa amri ya kuiondoa amri ya usimamizi.

Kumtembelea mtoto aliye chini ya amri ya uangalizi

**55.**-(1) Afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa-

(a) baada ya wiki ya kwanza ya kutolewa kwa amri ya usimamizi; na

(b) mara moja kila baada ya siku ishirini na nane baada ya ziara ya kwanza ya kipindi chote kilichotajwa kwenye amri ya usimamizi,

atamtembelea mtoto ambaye amewekwa chini ya uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa.

Maombi kwa ajili ya amri ya uondoaji

**56.** Pale ambapo-

(a) Mamlaka ya Serikali za Mitaa imefanya maombi kwa ajili ya amri ya usimamizi; na

(b) mkuu wa idara ya ustawi wa jamii anazo sababu za msingi kuamini kuwa mtoto anapata taabu au yuko hatarini kupata madhara na kwamba madhara hayo yasingekuwepo iwapo iwapo mtu aliyetajwa anaondolewa kutoka kwenye nyumba anayo mtoto;

(c) kuna mzazi au mtu mwingine kwenye nyumba hiyo ambaye yuko tayari kumpatia mtoto kiwango cha malezi ambayo yatahakikisha afya na maendeleo ya mtoto huyo, mamlaka ya serikali za mitaa inaweza kufanya maombi kwa mahakama kwa ajili ya kupata amri ya uondoaji.

(2) Maombi kwa ajili ya amri ya uondoaji yanaweza kufanywa kwa upande mmoja uliopo mahakamani au pande zote mbili zikiwepo mahakamani kwa mujibu wa kanuni za 146 hadi 147 za Kanuni za Mahakama ya Watoto.

(3) Mamlaka ya serikali za mitaa inaweza kuiomba mahakama amri -

(a) inayomtaka mtu aliyetajwa ndani yake kuondoka katika nyumba anayoishi;

(b) kumkataza mtu aliye tajwa kuingia kwenye nyumba au sehemu ambapo mtoto anaishi;

(c) kumzuia mtu aliyetajwa kuingia kwenye eneo lililotajwa lililo karibu na nyumba ambazo mtoto anaishi; au

(d) itakayomzuia mtu aliyetajwa kufanya mawasiliano na mtoto au watu wanaomlea mtoto kwa namna yoyote ile.

(4) Maombi yatataja kipindi ambacho amri ya uondoaji itahitajika, kipindi hicho hakitazidi siku ambayo mtoto atatimiza miaka kumi na minane.

(5) Maombi yanaweza kuiomba mahakama kucheleweshа utekelezaji wa mwenendo wa shauri la usimamizi wakati amri ya uondoaji bado inaendelea kutumika au katika muda ambao mamlaka ya serikali za mitaa itakapo ucheleweshaji huo kuondolewa au maombi kuondolewa.

(6) Wakati wowote ambao amri ya uondoaji bado inaendelea kutumika, maombi yanaweza kutofautiana nayo ili-

(a) kuwajumuisha watu wengine waliotajwa; au

(b) kuiondoa amri kuhusiana na mtu aliyetajwa; au

(c) kubadili muda wa amri hiyo kutumika.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## WAJIBU WA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MTAA KWA WATOTO WANAOHITAJI UANGALIZI

Wajibu kwa mtoto aliye chini ya amri ya uangalizi

**57.** Pale ambapo amri ya uangalizi inatolewa kuhusina na mtoto, itakuwa ni jukumu la mamlaka ya serikali za mitaa iliyotajwa kwenye amri hiyo kumpokea mtoto kwenye uangalizi wake.

Wajibu wa jumla wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa

**58.**-(1) Itakuwa ni wajibu wa jumla wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuchukua hatua muhimu ili kuhakikisha

kuwa, katika hali ya kawaida kabisa, kuwa kuna malazi ya kutosha ili kukidhi mahitaji ya watoto walio chini ya uangalizi wake.

(2) Mamlaka ya serikali za mtaa itazingatia manufaa ya kuwa na idadi zaidi ya moja ya watoa huduma ya malazi na maeneo tofauti ya malazi.

Wajibu wa jumla wa Idara ya Ustawi wa Jamii

**59**.-(1) Katika Kanuni hizi, rejea yoyote ya mtoto aliye chini ya uangalizi wa serikali za mtaa ni rejea kwa mtoto ambaye-

(a) yuko chini ya uangalizi wa muda au chini ya amri kamili ya mahakama;
(b) amewekwa chini ya uangalizi wa hiari kwa mujibu wa kanuni ya 42; au
(c) amepewa malazi na idara ya ustawi wa jamii katika utekelezaji wa yoyote kati ya majukumu yaliyotolewa kwake chini ya Sheria and chini ya kanuni ya 38.

(2) Mamlaka ya serikali ya mitaa itakuwa na jukumu, kuhusiana na mtoto aliye chini ya uangalizi wake-

(a) la kuhakikisha na kukuza ustawi wa mtoto huyo;
(b) la kumpatia mtoto malazi yanaofaa;
(c) la kumtunza mtoto; na
(d) la kukuza mafanikio ya kielimu na afya.

(3) Kabla ya kufanya uamuzi wowote mkubwa kuhusiana na mtoto aliye chini ya uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa, afisa ustawi wa jamii, kwa hali ya kawaida kabisa, atazingatia matakwa na hisia za-

(a) mtoto;
(b) wazazi wake; na
(c) mtu mwingine yeyote ambaye matakwa na hisia zake afisa ustawi wa jamii ataona ni muhimu, kwa kuzingatia suala linalotakiwa kuamuliwa.

(4) Katika kufanya muamuzi wowote, afisa ustawi wa jamii atazingatia-

(a) misingi iliyoainishwa chini ya kanuni ya 3; na
(b) matakwa na hisia za mtu mwingine yeyote aliyatajwa kwenye kanuni ndogo ya (4)(b) hadi (c) kwa kadri ambavyo zitakuwa zimethibitsha.

Haki ya mzazi na wajibu chini ya amri ya uangalizi

**60**.-(1) Pale ambapo amri ya uangalizi inatekelezwa kuhusiana na mtoto, mamlaka ya serikali za mtaa-

(a) itakuwa na haki za mzazi kuhusiana na mtoto huyo;
(b) itakuwa na uwezo wa kuamua kiasi ambacho mzazi au mlezi anaweza kutekeleza haki zake za uzazi kuhusiana na mtoto huyo.

(2) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, kwa niaba ya mamlaka ya serikali za mtaa ataweka ukomo kwenye utekelezaji wa haki za mzazi kwa kiasi ambacho ni muhimu kwa usalama wa mtoto na kwa ajili ya kukuza ustawi wa mtoto pekee.

(3) Wakati amri ya uangalizi inaendelea kutekelezwa-

(a) Mamlaka ya Serikali za Mitaa au mtu yeyote anayemuangalia mtoto-
 (i) hatabadili jina la mtoto; au
 (ii) hatamsababishia mtoto kubadili dini yake isipokuwa kwa amri ya mahakama;
(b) mamlaka ya serikali za mitaa , isipokuwa kwa idhini ya mahakama na kwa kipindi kisichozidi kipindi kilichoainishwa chini ya kanuni ndogo ya (4), hatamuondoa mtoto kutoka katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(4) Mtoto aliyewekwa chini ya uangalizi kufuatia amri ya mahakama, anaweza kusafiri nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi kisichozidi siku 28 chini ya uangalizi wa mzazi wake:

isipokuwa kwamba, mtu anayempeleka mtoto huyo amepata idhini ya maandishi ya mkuu wa idara ya ustawi wa jamii.

(5) Masharti ya kanuni ndogo ya (3)(b) hayatatumika iwapo amri ya uangalizi imetolewa kwa ajili ya mtoto kuishi nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Muda wa amri ya uangalizi

**61**.-(1) Kipindi cha juu zaidi kinachoweza kutolewa kwa amri ya uangalizi ni miaka mitatu au hadi ambapo mtoto atatimiza miaka kumi na minane.

(2) Mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atahakikisha kuwa mapitio kuhusu mtoto yanafanyika si zaidi ya miezi sita kabla ya tarehe ya kumuisha muda kwa amri ya uangalizi na ataamua , si zaidi ya miezi minne, kabla ya kuisha muda kwa

amri ya uangalizi -

(a) ama kuandaa mpango wa uondokanaji wa uangalizi ilikumsaidia mtoto atakapo ondoka chini ya uangalizi wa Mamlaka ya Serikali za Mtaa au la; au

(b) ama kufanya maombi kwenye mahakama ili kuongeza muda wa amri au la.

(3) Pale ambapo uamuzi wa mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii ni kufanya maombi ya kuongeza muda wa amri ya uangalizi, Mamlaka ya Serikali ya Mtaa itawasilisha-

(a) maelezo yatakayo ainisha sababu za kuongeza muda wa amri;

(b) uchunguzi wowote wa kijamii ambao uliofanywa na familia kwa madhumuni ya kuungana tena;

(c) mpango wa uangalizi unaoainisha maandalizi yanayotakiwa kufanyika kwa ajili ya mtoto, yatakayokuwa na taarifa zilizoainishwa kwenye kanuni ya 48;

(d) kumbukumbu ya mkutano wa mapitio iliyofanyika karibuni; na

(e) nakala ya amri halisi ya uangalizi na nyongeza zozote zilizofanywa kwenye amri halisi ya uangalizi.

(4) Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza kuomba nyongeza ya muda wa miaka mitatu.

(5) Hakutakuwa na ukomo wa idadi ya nyongeza ambazo amamlaka ya serikali za mitaa inaweza kuomba, isipokuwa kwamba, amri ya uangalizi itakwisha muda wake baada ya mtoto kutimiza umri wa miaka kumi na minane, iwapo atakuwa hajaachiliwa kabla ya tarehe hiyo.

Kumuhifadhi mtoto

**62.-**(1) Pale ambapo mtoto yuko chini ya uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa, mamlaka hiyo itakuwa na wajibu wa kumweka mtoto huyo kwenye sehemu ya malazi inayofaa.

(a) makazi chini ya uangalizi wa ndugu, rafiki au mtu anayehusiana na familia;

(b) makazi chini ya uangalizi wa mzazi wa kambo au mtu anayeaminika; au

(c) makazi kwenye makao yaliyoidhinishwa kwa mujibu wa Sheria.

(3) Afisa ustawi wa jamii-

(a) atatoa kipaumbele kwa makazi yanayoangukia chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (2)(a) kwa kulinganishwa na makazi yanayoangukia chini ya kanuni nyingine ndogo za kanuni hiyo; na
(b) hakikisha kuwa, pale inapobidi-
(c) yanaruhusu mtoto kuishi karibu na nyumba yake ya awali;
(d) hakikisha kuwa haiingilii elimu au mafunzo ya mtoto;
(e) hakikisha kuwa mtoto hatenganishwi na wadogo zake; na
(f) hakikisha kuwa, iwapo mtoto ana ulemavu, malazi yanayotolewa yanakidhi mahitaji maalum ya mtoto.

Kumtembelea mtoto aliye chini ya makazi ya hifadhi

**63**.-(1) Afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa atamtembelea mtoto aliyewekwa chini ya uangalizi wa Mamlaka ya Serikali ya Mitaa mara atakapopelekwa kwenye makao-
(a) si zaidi ya siku saba baada ya mtoto kupelekwa;
(b) si zaidi ya siku ishirini na nane baada ya ziara ya mara ya kwanza;
(c) kufuatia ziara ya pili, si chini ya mara moja kwa kila miezi mitatu kwa kipindi chote cha amri ya uangalizi;
(d) katika muda mwingine wowote ambao afisa aliye pangiwa au mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ataona unafaa.

(2) Pamoja na ziara zilziofanyika kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1), afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa, kwa kadri itakavyowezekana, atamtembelea mtoto pale atakapo hitajika kufanya hivyo na mtoto.

Kuendeshwa kwa ziara

**64**.-(1) Katika kila ziara, afisa ustawi wa jamii ataongea na mtoto kwa faragha, isipokuwa kama -
(a) mtoto, aliye na umri wa kuelewa na amepevuka, anakataa; au
(b) haiwezekani kufanya hivyo, kwa kuzingatia umri wa mtoto na kiwango chake cha uelewa.

(2) Afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa ataandaa taarifa ya maandishi ya ziara, ikijumuisha taarifa zinazoelelzea iwapo

makao hayo yanafaa na maoni na hisia za mtoto na ataweka kumbukumbu hiyo ya maandishi kwenye jalada la mtoto.

Kutoa taarifa kuhusu maoni ya eneo la makao

**65**.-(1) Pale ambapo, kutokana na ziara iliyoendeshwa kwa mujibu wa kanuni ya 63-

(a) afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa ana sababu za msingi kuamini kuwa ustawi wa mtoto hauzingatiwi ipasavyo na kukuzwa kwenye nyumba hiyo makazi, ataliwasilisha suala hilo kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii ndani ya saa arobaini na nane na mapitio yatafanyika kwenye makao hayo ya makao hayo;

(b) afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa anasababu za msingi kuamini kuwa mtoto yuko kwenye hatari ya moja kwa moja ya kupata madhara, anaweza kumtoa mtoto huyo kutoka kwenye nyumba hiyo ya makazi wakati mapitio ya makazi hayo yana unasubiriwa;

(2) Pale ambapo kanuni ndogo ya (2) itatumika na makazi ya mtoto yanafanyiwa mapitio au kufutwa uchunguzi wa utafanyika kwa watoto wengine wanaoshi kwenye makao hayo.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
### MAPITIO KUHUSIANA NA WATOTO WALIO CHINI YA UANGALIZI AU USIMAMIZI WA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MTAA

Mapitio

**66.-**(1) Mapitio ya mara kwa mara yatafanyika kuhusiana na kila mtoto aliye chini ya uangalizi au aliye chini ya usimamizi wa mamlaka ya serikali za mitaa kutokana na-

(a) amri ya uangalizi au amri ya usimamizi iliyotolewa na mahakama;

(b) amri ya muda ya uangalizi au usimamizi iliyotolewa na mahakama;

(c) mtoto kupotea, kutelekezwa, kutafuta hifadhi au wazazi wake hawawezi kupatikana; au

(d) mtoto kuwekwa chini ya uangalizi wa hiari kwa idhini ya wazazi.

(2) Mapitio yatatathmini iwapo mpango wa huduma ya uangalizi uliopo unakidhi mahitaji ya mtoto na iwapo kuna mabadiliko yoyote yanayohitajika.

(3) Mkuu wa idara ya ustawi wa jamii atachukua jukumu la kuhakikisha kuwa mapitio yanafanyika kwa watoto wanaoangukia chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (1).

(4) Mapitio ya kwanza yatafanyika si zaidi ya siku ishirini na nane, baada ya mtoto kuwekwa chini ya uangalizi au usimamizi wa mamlaka ya serikali za mitaa.

(5) Mapitio ya pili yatafanyika si zaidi ya miezi mitatu baada ya mapitio ya kwanza na mapitio yatafanyika kila baada ya miezi sita baada ya hapo mtoto atakoma kuwa chini ya uangalizi au usimamizi wa mamlaka ya serikali za mitaa isipokuwa kwamba-

(a) kutakuwa na mapitio ya kila mwezi kabla ya kuisha kwa muda wa kila amri ya usimamizi; na

(b) kutakuwa na mapitio si zaidi ya miezi sita kabla ya tarehe ya kuisha muda kwa amri ya usimamizi ili kuamua iwapo maombi ya ziada kwa ajili ya amri ya uangalizi kuongezewa muda yanapaswa kufanyika chini ya kanuni ya 61(2).

(6) Mapitio ya pili ya mapitio yatakayofuata yatasimamia utekelezaji wa mpango wa uangalizi au mpango wa usimamizi na kufanya marekebisho kwenye mpango huo kwa akadri itakavyokuwa muhimu ili kuonyesha taarifa mpya na mambo yoyote yaliyobadilika.

(7) Idara ya Ustawi wa Jamii hatafanya mabadiliko yoyote kwenye mpango wa uangalizi au usimamizi isipokuwa kama mabadiliko yanayokusudiwa kwanza yamezingatiwa wakati wa kufanya mapitio ya shauri la mtoto, isipokuwa iwapo kikawaida haiwezekani kufanya hivyo au ni kwa manufaa ya mtoto.

(8) Mapitio yanaweza kufanyika mapema zaidi kabla ya tarehe zilizoainishwa na kanuni hii iwapo-

(a) maamuzi yaliyokubalika kutokana na mapitio hayajatekelezwa ndani ya muda uliotajwa;

(b) iwapo ni kwa mtoto aliye chini ya uangalizi wa serikali ya mitaa, kuna mabadiliko ya msingi kuhusiana na maandalizi ya namna ambavyo mzazi, mlezi au mwangalizi wa zamani au watu wengine muhimu katika maisha ya mtoto wataweza kuonana naye;

(c) kuna mabadiliko ya afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa;

(d) kuna wasiwasi kuhusiana na usalama wa mtoto huyo;
(e) kuna malalamiko kutoka kwa au kwa niaba ya mtoto, mzazi au mwangalizi;
(f) kuna mabadiliko yasiyotarajiwa kuhusiana na makazi ya mtoto ikijumuisha mtoto kuwekwa mahabusi kutumikia kifungo katika Shule ya Maadilisho na mahakama;
(g) kuna mabadiliko katika mazingira ya kifamilia kama vile kuzaliwa au uzazi, ndoa au kifo ambavyo vinaweza kuwa na athari maalum kwa mtoto;
(h) mtoto ameshitakiwa kwa kosa la jinai;
(i) mtoto ametengwa shuleni;
(j) kuna sababu za msingi za kiafya, matukio ya kitabibu, utambuzi wa ugonjwa, ugonjwa, kulazwa au ajali kubwa zilizo na athari maalum kwa mtoto;
(k) mtoto ametelekezwa au ametoweka kutoka katika sehemu yake ya makazi.

(9) Pale ambapo mtoto ametoroka au haonekani katika sehemu yake ya makap, hatarudishwa kwenye sehemu yake ya makao hadi hapo amehojiwa na afisa ustawi wa jamii kuhusiana na sababu zilizosababisha kutoroka na mapitio yaliyofanyika iwapo mtoto atadai kuwa alikuwa anadhalilishwa, ametelekezwa au anatumiwa kwa namna isiyostahili katika sehemu hiyo makao.

(10) Mapitio yatafanyika kabla mtoto hajapelekwa kwenye taasisi iliyotajwa au chini ya ulinzi kwa kutenda kosa la jinai.

Utaratibu wa mapitio ya awali

**67**.-(1) Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii atamteua mjumbe wa idara ya ustawi wa jamii, mbali na afisa wa ustawi wa jamii aliyepangiwa kwa mtoto huyo, kuwa mwenyekiti wa mapitio.

(2) Mwenyekiti wa mapitio na afisa aliye pangiwa watakutana si zaidi ya siku kumi kabla ya mapitio ili kuamua -
(a) nani atakayealikwa kwenye mapitio;
(b) muda na mahali ambapo mapitio yatafanyika;
(c) maandalizi kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa kuhusiana na mtoto kwa wataalam watakaohudhuria; na

(d) iwapo taarifa itapelekwa kwa watu maalum, taasisi au vyombo ili kuwataka kuhudhuria.

Wajumbe wa mapitio

**68**.-(1) Wajumbe wa mapitio watajumuisha afisa wa ustawi wa jamii aliyeteuliwa na wanaweza kujumuisha-

(a) mtu anaye mlea mtoto, iwapo mtoto yuko chini ya uangalizi wa ndugu au rafiki wa familia;

(b) iwapo mtoto yuko kwenye malezi yakambo au yuko chini ya uangalizi wa mtu anayeaminika kumtunza, mzazi wa kambo wa mtoto au mtu anayeaminika kumwangalia;

(c) iwapo mtoto amewekwa kwenye makao makao yaliyothibitishwa au mwakilishi wa makao ya kulelea watoto;

(d) mwalimu, daktari, mtaalam wa saikolojia wa mtoto, au mtaalam mwingine aliye na mawasiliano na mtoto;

(e) idadi ya maafisa wa mamlaka ya serikali za mitaa, kwa kadri ambavyo mkuu wa idara yaustawi wa jamii ataona inafaa;

(f) mtu mwingine yeyote ambaye mwenyekiti anaamini kuwa ni muhimu kwa ajili ya malezi ya mtoto; na

(g) mtoto, iwapo ametimiza umri wa kuelewa na umri wa utu uzima.

(2) Maoni ya maandishi au taarifa, pale zitakapohitajika, zita tafutwa na kupatikana kwa muda mzuri ili ziweze kuzingatiwa kama sehemu ya mkutano wa mapitio.

(3) Pale ambapo afisa wa ustawi wa jamii aliyepangiwa anaamini kuwa mahudhurio ya amtu aliye tajwa, taasisi au chombo ni muhimu, atamtaarifu mwenyekiti ambaye atatoa taarifa kwa mtu huyo, taasisi au chombo si zaidi ya siku saba kabla ya mkutano wa mapitio kuwa wanatakiwa kuhuduria.

(4) Pale ambapo mtoto yuko chini ya uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa, mzazi, mlezi au mwangalizi atataarifiwa kuhusu mkutano wa mapitio, isipokuwa hawataalikwa kuhudhuria mahojiano tu, iwapo ni kwa maoni ya afisa ustawi wa jamii kuwa kufanya hivyo ni kwa manufaa ya mtoto.

(5) Pale ambapo inagundulika kuwa, ni kwa manufaa ya mtoto kuwa mzazi, mlezi au mwangalizi wahudhurie, mzazi atakuwa na haki ya kuambatana na wakili, rafiki au mtetezi kwa ajili ya kuwasaidia wakati wa mapitio.

(6) Pale ambapo mtoto yuko chini ya uangalizi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mzazi, mlezi au mwangalizi ataalikwa kuhudhuria na atakuwana haki ya kuambatana na wakili, rafiki au mtetezi kwa ajili ya kuwasaidia wakati wa mapitio.

(7) Pale ambapo mzazi, mlezi au mwangalizi hawajaalikwa au hawawezi au hawataki kuhudhuria mkutano wa mapitio mzazi, mlezi au mwangalizi huyo ataruhusiwa kuwasilisha maelezo ya maandishi au ya mdomo kwa kupitia wakili rafiki au mtetezi au mjumbe wa mkutano, mbali na mtoto.

Mahudhurio ya mtoto katika mkutano wa mapitio

**69**.-(1) Afisa aliyepangiwa, si zaidi ya siku kumi na nne kabla ya mkutano wa mapitio, atakutana na mtoto ili kujua iwapo kuna mtu yeyote ambaye mtoto angependa ahudhrurie mkutano, na iwapo mtoto menyewe hataki kuhudhuria, maoni na matakwa ambayo mtoto angependa wajumbe wa mkutano wa mapitio wayajue.

(3) Iwapo mtoto anataka kuhudhuria mkutano wa mapitio, isipokuwa hawezi kumpata wakili, rafiki au mtetezi ili ahudhurie naye, afisa ustawi wa jamii atafanya juhudi zote kwa kadri ya uwezo wake ili kumpata mtu atakaye msaidia mtoto huyo.

Taarifa kwa ajili ya mapitio

**70**.-(1) Afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa, ndani ya siku saba baada ya mkutano wa mapitio, atawasilisha kwa wajumbe wataalam na mzazi, mlezi au mwangalizi, iwapo wamealikwa, taarifa ya maandishi kuhusu-

(a) maendeleo ya mtoto;

(b) mabadiliko yoyote yatakayohitajika kuhusiana na hadhi ya kisheria ya mtoto, ikijumuisha kusudio lolote la kufanya maombi kwa ajili ya amri ya uangalizi au amri ya kufuta amri ya uangalizi.

(2) Afisa ustawi wa jamii aliyepangiwa ata-

(a) atawasilisha kwa wajumbe wataalam taarifa yoyote ya maandishi kuhusu uangalizi wa mtoto na kutoka kwa wataalam wanaohusika na mtoto

kuhusiana na maendeleo ya mtoto ama kabla au wakati wa mkutano;

(b) atahakikisha kuwa maoni na matakwa ya mtoto yanawekwa wazi wakati kwenye mkutano wa mapitio, iwapo mtoto hataki kuhudhuria mkutano wa mapitio, hana umri wa uelewa na wa utu uzima kuhudhuria mkutano wa mapitio au inachukuliwa kuwa ni kwa manufaa ya mtoto kuhudhuria mkutano wa mapitio; na

(c) atatoa taarifa kwa mtu yeyote, taasisi au chombo kinachotakiwa kuhudhuria mkutano wa mapitio.

Jukumu la mwenyekiti wa mkutano wa mapitio

**71**.-(1) Jukumu la mweyekiti litakuwa ni -

(a) kuhakikisha kuwa watu wote wanaohudhuria mkutano wanelewa dhumuni lake na yatakayojiri;

(b) kupanga agenda za mkutano;

(c) wakumbusha wahusika wote kuwa mkutano wa mapitio ni wa siri;

(d) kuwawezesha wahusika wote waliopo kutoa michango kikamilifu wakati wa majadiliano na wakati wa kufanya uamuzi; na

(e) kuhakikisha kuwa mapitio yanazingatia taarifa zote zilizowasilishwa na maoni ya wahusika wote na matakwa ya mtoto.

(2) Kanuni ya 32 itatumika katika mikutano ya mapitio.

Kumbukumbu ya mapitio

7**2.-**(1) Nyaraka zitawasilishwa kwa wahusika watakaohudhuria mkutano wa mapitio, mbali na taarifa ya afisa ustawi wa jamii iliyotolewa chini ya kanuni ya 70(1), hazitazuiliwa baada ya mapitio au kuondolewa kwenye chumba cha mkutano ambamo mkutano wa mapitio unafanyika, mbali na kwa wataalam wanaomshughulikia mtoto.

(2) Nyaraka zote na kumbukumbu zozote za mapitio zitakuwa siri na hazitatolewa kwa watu walio nje ya mkutano wa mapitio bila idhini ya mkuu wa idara ya ustawi wa jamii au amri ya mahakama.

(3) Mwenyekiti atahakikisha kuwa kuna mahudhurio ya mtu anayefaa kuchukua kumbukumbu za mkutano ambazo zita-

(a) sambazwa kwa wataalam wote wanaohudhuria

mkutano isipokuwa, wahusika watazitachukulia kuwa ni siri;

(b) idhinishwa na kusainiwa na mwenyekiti wa mkutano wa mapitio;

(c) kuwa na mapendekezo ya mkutano wa mapitio;

(d) pelekwa kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii; na

(e) itawekwa kwenye jalada la mtoto.

(3) Mzazi, mlezi au mwangilizi watapatiwa nakala ya maandishi ya mapendekezo ya mkutano wa mapitio ya mtoto.

(4) Mpango wa uangalizi wa mtoto utafanyiwa marekebisho kwa mujibu wa uamuzi wa mkutano wa mapitio.

Mapitio ya pili na yatakayofuatia

**73**.-(1) Mapitio ya pili na yatakayofuatia yatazingatia-

(a) madhara ya mabadiliko yoyote katika maendeleo ya mtoto kutokea mapitio ya mwisho;

(b) iwapo maamuzi yaliyochukuliwa katika mapitio ya mwisho yametekelezwa ipasavyo, na iwapo bado, sababu za kutokutekelezwa huko;

(c) iwapo iadara ya ustawi wa jamii itahitaji mabadiliko yoyote katika hadhi ya kisheria ya mtoto, ikijumuisha maombi kwa ajili ya amri ya uangalizi au usimamizi au ya kufutwa kwa amri ya uangalizi au ya usimamizi;

(d) iwapo kuna mpango wa utekelezaji wa kudumu;

(e) iwapo, kama ni kuhusiana na mtoto aliye chini ya uangalizi wa mamlaka ya serikali za mitaa, kuna haja ya kubadilisha utaratibu kwa ajili ya namna ya kuonana kati ya mtoto na familia yake au ndugu wengine muhimu;

(f) iwapo kuwekwa kwa mtoto chini ya malezi kunaendelea na iwapo kunakidhi matakwa/mahitaji ya mtoto;

(g) mahitaji ya kieleimu ya mtoto na iwapo taratibu zilizopo zinakidhi mahitaji ya kieleimu ya mtoto au yanahitaji kufanyiwa marekebisho;

(h) afya ya mtoto, ikijumuisha kipaumbele katika mahitaji ya afya ya mwili na afya ya akili na iwapo taratibu zilizopo zinakidhi mahitaji ya kielimu ya mtoto au yanahitaji kufanyiwa mabadiliko;

(i) matakwa na hisia za mtoto kuhusu mpango wa uangalizi, ikijumuisha, kuhusiana na mabadiliko yoyote au mabadiliko yanayopendekezwa kuhusiana na mpango wa uangalizi au usimamizi kwa kuzingatia umri wa mtoto na kiwango chake cha utu uzima**.**

Mapitio ya mpango wa uangalizi kufuatia mapitio

**74**. Kufuatia mapitio, idara ya ustawi wa jamii itatoa nakala ya mpango wowote wa uangalizi uliopitiwa, kurekebishwa kwa-

(a) mtoto;
(b) mzazi;
(c) ndugu yeyote au rafiki wa familia ambaye mtoto yuko chini ya uangalizi wake;
(d) iwapo mtoto yuko chini ya malezi yakambo, mzazi wa kambo au familia;
(e) iwapo mtoto amewekwa kwenye makao iliyoidhinishwa, mkuu wa makao hayo iliyoidhinishwa;
(f) iwapo mtoto amewekwa chini ya ulinzi, kwa mkuu wa shule maadilisho au taasisi nyingine.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
### KUONDOLEWA KWA AMRI YA UANGALIZI

Kuondolewa kwa amri ya uangalizi Tangazo la Seriklai......

**75.**-(1) Mamlaka ya serikali za mtaa inaweza kufanya maombi kwa ajili ya amri ya kufuta amri ya uangalizi chini ya kanuni ya 134 ya Kanuni za Mahakama ya Watoto iwapo inaamini kuwa amri hiyo haihitajiki tena kwa ajili ya kumlinda mtoto dhidi ya madhara au madhara ya kiafya au maendeleo kama ilivyo tafsiriwa na kanuni ya 4.

(2) Pale ambapo Mamlaka ya Serikali za Mitaa inafanya maombi kwa ajili ya amri ya kufuta amri ya uangalizi, mtoto na wazazi au mlezi watatajwa kama wahusika katika mwenendo na mlezi aliyeteuliwa na mahakama kwa mtoto.

(3) Wakati wa kufanya maombi kwa ajili ya amri ya kuondoa amri ya uangalizi, mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii, kwa niaba ya Mamlaka ya Serikali za Mtaa, ataandaa na kuwasilisha maelezo na mpango wa uangalizi.

(4) Mpango wa uangalizi utajumuisha masharti

kuhusiana na taarifa kuhusu-

(a) mahali ambapo mtoto ataishi na atataishi na nani baada ya kutolewa kwa amri ya kuondoa amri ya uangalizi;

(b) msaada ambao utakaotolewa kwa mtoto kutoka kwa wazazi wake au watu wengine kufuatia kuondolewa chini ya uangalizi;

(c) vyanzo vyamapato vya mzazi, mlezi au muangalizi na mtoto;

(d) hali ya kiafya ya mtoto;

(e) hitaji endelevu la mtoto kupata elimu, mafunzo na ajira;

(f) matakwa na hisia za mtoto, mzazi yeyote au mlezi na mtu mwingine yeyote ambaye anatarajiwa kukaa na mtoto;

(g) huduma,iwapo zipo, zitakazotolewa na idara ya ustawi wa jamii.

(5) Pale ambapo mahakama inaondoa amri ya uangalizi, afisa ustawi wa jamii ata-

(a) mtembelea mtoto si zaidi ya siku saba baada ya kutolewa kwa amri;

(b) si zaidi ya siku 28 baada ya ziara ya kwanza;

(6) Pale ambapo mtoto anaishi kwenye serikali ya mitaa, mbali na ile ambayo amri ua uangalizi ilitolewa kwake, mkuu wa idara ya ustawi wa jamii, pale itakapowezekana kufanya ziara, ataiomba Idara ya Ustawi wa Jamii ya mamlaka ya serikali ya mitaa mpya kufanya ziara kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (5) na kuwasilisha taarifa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (8).

(7) Kufuatia ziara ya pili, afisa ustawi wa jamii atafanya mapitio kwenye mpango wa uangalizi ilikuamua iwapo ni muhimu kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya mtoto na iwapo mtoto anahitaji msaada zaidi au hatua za ziada na atawasilisha taarifa ya maandishi kuhusu maoni/matokeo yake kwa mkuu wa idara ya ustawi wa jamii.

(8) Pale ambapo taarifa ya kuondolewa-

(a) inapendekeza hatua za ziada zisizo kuwa ndani ya mpango wa uangalizi uliofutwa kutolewa, Idara ya Ustawi wa Jamii itapeleka suala hilo kwenye idara ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi;

(b) inapendekeza hatua za ziada kwa ajili ya

kutunza/kuhifadhi ustawi wa mtoto, mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii atazingatia-

(i) iwapo suala lipelekwe kwenye mkutano wa usalama wa mtoto; au`

(ii) iwapo maombi kwa ajili ya huduma ya ziada ya uangalizi au ya usimaizi yanahitajika.

Oktoba...........2014

MHE. HADJI H. MPONDA,
*Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii*